UKURASA WA 2
**Binti** adaiwa kuua kichanga akaishi huru kwa mama yake Dar



UKURASA WA 5
**Mikoa** mitano inayoongoza wakazi kukosa vyoo hii hapa





GABRIEL JESUS KUICHEZEA BRAZIL DHIDI YA ARGENTINA

UKURASA 22


# Nipashe

Jumanne Novemba 21, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581501

nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com




# Simbachawene alia rushwa imetapakaa

UKURASA 2

UKURASA WA 5
## TEA YAJENGA ZAIDI YA MADARASA 300 KIPINDI CHA SAMIA
MAMLAKA ya Elimu Tanzania (TEA), imesema katika kipindi cha uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan...

UKURASA WA 7
## MVUA YASABABISHA VIFO VYA WATU 2
MKUU wa Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara, Kheri James, amesema...

UKURASA WA 19
## IRAN YAJA NA HOJA ISRAEL KUTENGWA
KIONGOZI Mkuu wa Kidini wa Iran, Ayatollah Ali Khamenei, ametoa wito kwa mataifa ya Kiislamu yenye...

## Mwinyi akerwa ugomvi viongozi ofisini
UKURASA 3



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Magomeni, wilayani Tunduru, mkoani Ruvuma wakiwa darasani Oktoba 30 mwaka huu. **Picha ndogo chini** ni mwonekano wa darasa lingine katika shule hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



MADARASA YA NYASI
## Ukweli kuanikwa; DC, DED waamua kuyavunja
• **Wajitetea** ufumbuzi wake bajeti ya bilioni 18/-... *Endelea ukurasa 4*

**MICHEZO** STARS, MOROCCO NI USHINDI TU LEO UK.24 **KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan akiongoza kikao cha Baraza la Mawaziri kilichofanyika Ikulu Chamwino, Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Simbachawene alia rushwa imetapakaa kona za serikali

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, George Simbachawene, amekiri hali bado si nzuri kutapakaa kwa kashfa ya rushwa ndani ya mifumo ya kiserikali, hata kuathiri ufanisi wa huduma.

"Bado suala la rushwa ndogondogo ni tatizo sana kwa wananchi wetu na huko ndiko yako malalamiko mengi ya watu kutokana na rushwa hiyo kuwanyima fursa ya kupata huduma," alisema waziri huyo jana.

Ni kauli aliyoitoa alipofungua mkutano mkuu wa mwaka wa viongozi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Alisema bado yapo malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kuwapo rushwa katika taasisi mbalimbali hali inayosababisha wananchi kukosa huduma ambazo wanazihitaji.

"Huduma hizo ni pamoja na elimu ngazi za chini, kati hadi vyuo vikuu, lakini huduma za afya, kodi na leseni ambako kumewekwa utaratibu mgumu na ukiritimba katika utoaji huduma ili tu watu watoe rushwa ndipo wahudumiwe," alifanua.



Waziri Simbachawene alisema kuwa kutokana na hali hiyo, kila taasisi inatakiwa kutengeneza mkataba wa huduma kwa wateja na TAKUKURU iwe nao kama sehemu ya kufuatilia utekelezaji wake.

"Tukitoka tu hapa tukaenda pale Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma (General) tukajificha mahali na kuangalia namna shughuli zinavyoendelea kama ni mhudumu au daktari atakuwa anatoa huduma bora, tutaona.

"Na kama kuna mhudumu ambaye atakuwa hatoi huduma bora tutabaini hivyo. Hizi rushwa ndogondogo zinakera sana wananchi kuliko hata hizi za ubadhirifu wa mabilioni ambayo wao hawayaoni," alisisitiza.

Simbachawene alisema TAKUKUTU inapaswa kuendeleza kushughulikia watu wote ambao watabainika kujihusisha na vitendo vya rushwa nchini bila kuangalia hali zao.

"Lazima tuwashughulikie watu wote wanaojihusisha na rushwa nchini. Zipo rushwa zinaonekana kabla ya kukamilika kwa miradi, lakini zipo ambazo zinaanza kuonekana baada ya miaka mitatu tangu kukamilika kwa mradi.

"Hivyo, wahusika wote wanatakiwa kukamatwa na kuhojiwa hata kama watakuwa wamestaafu," aliagiza Waziri Simbachawene.

Alisema hali hiyo itasaidia kukomesha tabia zinazofanywa na baadhi ya watumishi wa umma kwa kujihusisha na rushwa na kuhama kituo cha kazi.

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Salum Hamduni, alisema mkutano huo wa siku tatu unalenga kujadili mafanikio na changamoto kwa mwaka uliopita ili kuzipatia suluhu.

Hamduni alibainisha kuwa mwaka uliopita, taasisi hiyo iliokoa Sh. bilioni 171.9 ambazo zingeingia mifukoni mwa watu kama isingefanya operesheni mbalimbali kwenye miradi ya umma.

Alisema mkutano huo utatoka na maazimio ambayo watakwenda kuyafanyia kazi ili kupunguza malalamiko ya wananchi kuhusu vitendo vya rushwa katika sehemu mbalimbali nchini.

Ripoti ya Uwajibikaji ya Viashiria vya Rushwa, Ubadhirifu na Udanganyifu 2021/22 iliyoandaliwa na Taasisi ya WAJIBU kutokana na ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) za ukaguzi wa Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Mamlaka ya Serikali za Mitaa za mwaka wa fedha 2021/22, inabainisha miamala mbalimbali yenye viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu wa fedha za umma.

Kwa mwaka wa fedha 2021/22, uchambuzi umeonesha kuna viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu katika matumizi ya kawaida, mishahara, mafao na rasilimali watu yenye thamani ya Sh. bilioni 411.31 yaliyotokana na kasoro mbalimbali.

Uchambuzi huo unaonesha dosari hiyo imepungua kwa asilimia 63 kutoka Sh. trilioni 1.14 mwaka wa fedha 2020/21 mpaka Sh. bilioni 411.31 mwaka wa fedha 2021/22.

## Adaiwa kunyonga mwanawe ili aende Dar

**Na Francis Godwin,** IRINGA

JOHARI Mbuma (19), mkazi wa Mawelewele, Kata ya Mwangata, Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kumuua mtoto wake mwenye umri wa miezi tisa kwa kumnyonga kisha kumtumbukiza kwenye ndoo ya maji chooni, ili aende Dar es Salaam kuishi na mama yake mzazi.

Akihojiwa na uongozi wa Mtaa wa Mawelewele mjini Iringa, Johari alidai amekuwa anaishi maisha magumu. Baada ya kuwasiliana na mama yake, alimtaka aende kuishi jijini Dar es Salaam, lakini kukawa na masharti kwamba atapaswa kwenda pekee yake bila mtoto.

"Mama alisema kwa kuwa nimekatisha masomo kutokana na ujauzito na ninataka kwenda kuishi naye Dar es Salaam, basi niende mwenyewe bila mtoto na kama nitakwenda na mtoto nisifikie nyumbani kwake, ndio maana nikalazimika kumnyonga mtoto wangu na kumtupa kwenye ndoo ya maji ili nisafiri kwenda kuishi na mama Dar es Salaam," alidai Johari.

Alidai kuwa kabla ya kupata wazo la kuua mtoto huyo alikwenda kwa rafiki yake kwa lengo la kumtelekeza huko mtoto huyo, lakini alimkosa na ndipo aliamua kumnyonga na kumtumbukiza kwenye ndoo ya maji iliyokuwa kwenye choo cha nyumbani kwa rafiki yake.

Alidai kuwa mwanaume aliyezaa naye anaishi Pawaga, Wilaya ya Iringa na tangu alipobaini kuwa ana ujauzito, hajawahi kuwasiliana naye wala kumhudumia kwa chochote.

Alidai kuwa kutokana na maisha magumu, alimpigia mama yake mzazi na kumwomba msamaha kwa kukatisha masomo ya sekondari kwa sababu ya ujauzito.

Johari alikuwa miongoni mwa wanafunzi wa kidato cha nne wanaotarajiwa kuhitimu masomo yao mwaka huu, lakini kutokana na ujauzito alikatisha masomo.

Bibi wa Johari, Chiku Mbuma, akizungumzia tukio hilo, alidai tukio la ukatili dhidi ya mtoto huyo lilitendwa juzi. Mchana wa Jumamosi (siku moja kabla ya mauaji)walikutana na mjukuu wake huyo akiwa na mtoto mgongoni na hakumweleza chochote kuhusu kuitwa na mama yake Dar es Salaam.

Alisema alishangazwa kuitwa katika ofisi ya Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa na kuelezwa juu ya kushikiliwa kwa Johari kutokana na tuhuma za kuua mtoto wake.

Katibu wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Wilaya ya Iringa Mjini, Faima Mohamed, alisema alijulishwa juzi mchana kuhusu tukio la kukutwa maiti ya mtoto chooni, lakini mhusika wa tukio hilo hawakumkuta.

Alisema kuwa kutokana na mhusika wa mauaji hayo kutojulikana, waliendelea kufanya msako kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi hadi jana asubuhi walipompata mhusika huyo.

Diwani wa Viti Maalum, Kata ya Mwangata, Devotha Chaula, alisema mtuhumiwa wa mauaji hayo alikamatwa jana asubuhi baada ya kurudi kwenye mtaa alikotupa mwili wa mwanawe huyo. Alidai alirejea huko kwa lengo la kuuchukua ili akautupe vichakani.

"Kwa kuwa toka jana tuliweka mkakati wa kumsaka binti aliyehusika na mauaji hayo wananchi na viongozi tulitawanyika kwenye mitaa mbalimbali kumtafuta mhusika, asubuhi tulipomwona binti huyo akiwa eneo la tukio, tulimkamata na kumhoji. Bila kukataa alikubali kuwa ni yeye aliyefanya unyama huo," alidai.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mawelewele, Obed Mtatifikolo, alithibitisha kukamatwa mtuhumiwa huyo na kuwa tayari amekabidhiwa polisi kwa hatua zaidi za kisheria.

HABARI KITAIFA

# Mwinyi akerwa na viongozi kulumbana

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema hafurahishwi na vitendo vya baadhi ya viongozi katika serikali yake kulumbana wenyewe kwa wenyewe badala ya kufanya kazi ya kuwatumikia wananchi.

Akizungumza jana, Ikulu Zanzibar, katika hafla ya kuwaapisha wakuu wa wilaya na mikoa aliowateua hivi karibuni, alisema moja ya tatizo kubwa ni viongozi wa serikali kugombana wenyewe kwa wenyewe hali ambayo haileti ufanisi wa kazi katika kuwatumikia wananchi.

Aliwataka watendaji wote aliowateua kufanya kazi kwa ushirikiano na watendaji wenzao na kuachana na malumbano yasiyo na faida yoyote.

"Ipo changamoto ya mawaziri kugombana na makatibu wakuu, au makatibu wakuu kugombana na wakurugenzi, au wakuu wa mikoa kugombana na wakuu wa wilaya au makatibu tawala jambo hili halileti taswira nzuri katika nchi yetu twendeni tukawatumikie wananchi na sio malumbano," alisema Dk. Mwinyi.

Rais Mwinyi alisema haypo tayari kuona vitendo hivyo vinaendelea na watu ambao hawawezi kufanya kazi kwa pamoja na kwamba hatosita kuchukua hatua kwa sababu hawafai katika uongozi wake.

"Ifike sehemu mkiwa hamuwezi kufanya kazi kwa pamoja basi tuambizane mapema ili tuitane tuzungumze kwa sababu ugomvi na mabifu yamekuwa mengi na tunaharibu kazi kwa wananchi," alisema Dk. Mwinyi akioneshwa kukerwa na jambo hilo.

Aidha, Rais Mwinyi aliwataka wakuu wa mikoa na wilaya kuhakikisha wanasimamia ulinzi na usalama katika maeneo yao na inapaswa kuwa ndio kazi ya msingi kuliko zote ili maeneo yote yawe salama.

Rais Mwinyi alisema hivi karibuni kumejitokeza hali ya uvunjifu wa usalama kwa kasi katika maeneo mbalimbali hususan ya utalii ikiwamo Nungwi na Paje na kupokea taarifa za kiusalama zikionesha matukio mengi.

"Nataka mkahakikishe kwamba mkiwa wenyeviti wa kamati zenu za ulinzi na usalama za mikoa na wilaya, basi matukio haya hayaongezeki bali yanashughulikiwa kwa nguvu zote, hakikisheni hali ya ulinzi katika maeneo yetu yanakuwa mazuri wakati wote," alisema.

Pia Dk. Mwinyi alitoa maagizo kwa viongozi hao kutatua kero za wananchi na kuwasikiliza katika maeneo yao kwasababu zipo kero na changamoto nyingi zinazohitaji ufumbuzi.

"Hakikisheni mnarekebisha kasoro zinazotokea katika mambo ya ardhi na wajibu wenu ni kutenda haki na msiwe sehemu ya kero hizo kwani kutoshughulikiwa kikamilifu na wakati kero hizi zinanifika mimi na wakati mwingine viongozi wanahusika katika hilo lisiwe tatizo tena mshughulikie," alisema.

Alisema, Zanzibar ni nchi ya utalii na zaidi ya theluthi moja ya pato la taifa linatokana na utalii na kwamba utalii ni nguzo kuu ya uchumi wa nchi hivyo ni vyema viongozi wakatatua kero za wawekezaji ikiwamo kutoshughulikiwa kikamilifu katika ngazi za wilaya na mikoa.

"Wapo watu ambao kwa makusudi kabisa wanaondoa haki za wawekezaji hao ni lazima kuhakikisha wanapewa haki zao na wao kuwa ni sehemu ya utatuzi wa changamoto zao," alisema.

Aliwataka, kusimamia halmashauri na manispaa kutokana na kuwapo kero nyingi zinazohusu wajasiriamali wadogo ikiwamo suala la usafi wa mazingira.

Alisema wapo baadhi ya masheha hawafanyi wajibu wao na wakurugenzi katika halmashauri na kuwataka kusimamia wajibu na majukumu yao.

"Lazima mwangalie haki inatendeka kwa sababu zipo kesi zinakuja kwangu na unaona hasa haki inapindishwa kalisimamieni hili," alisisitiza.

Viongozi walioapishwa walisema watahakikisha wanasimamia maagizo yote waliyopewa na mkuu wao wa nchi na kufuata miongozo ya utendaji wao wa kazi, ili kero zote za wananchi zinazojitokeza zitatuliwe.

Walioapishwa ni Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, kabla ya uteuzi huo alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Rashid Hadid Rashid, Mkuu wa Mkoa wa Kaskazuini Unguja ambaye kabla ya uteuzi huo alikuwa ni Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja.

Wengine ni Sadifa Juma Khamis, Mkuu wa Wilaya ya Kati kabla ya uteuzi alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini 'A', Othman Ali Maulid Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini 'A' na Galos Nyimbo ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja.



# Waziri aonya waganga wakuu vifo wajawazito

**Na Pilly Kigome**

WAGANGA wakuu wa mikoa na wilaya nchini kote wametakiwa kuwa macho kuepukana na vifo vya kizembe vitokanavyo na uzazi.

Amesema uzembe utawafanya wawe watuhumiwa namba moja katika vifo hivyo vitakavyotokea kwenye maeneo yao ya kazi.

Agizo hilo lilitolewa jana na Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel wakati wa ziara yake katika Hospitali za Rufani za mikoa za Temeke na Mwananyamala.

Dk. Mollel alisema vifo vitakavyogundulika ni vya kizembe katika hospitali yoyote nchini, wakuu hao na watumishi waliosababisha kifo watachukuliwa hatua kali, ikiwamo kusimamishwa kazi na kuwa chini ya ulinzi hadi hapo uchunguzi utakapokamilika.

"Hii itakuwa chachu ya kuwa makini kazini na kila mmoja kuwajibika eneo lake la kazi na si kuwaachia wachache.

"Hatuwezi kupoteza nguvukazi ya Taifa kwa uzembe wa watu wachache ambao wamekuwa hawawajibiki kazini," alionya Dk. Mollel.

Alisema serikali inataka kuhakikisha huduma bora katika sekta ya afya na sasa wizara imekuja na kaulimbiu ya kutaka ubora wa afya sambamba na ubora wa huduma.

Mbali na angalizo hilo, pia aliwataka viongozi wote wanaoongoza hospitali hizo kuboresha huduma kwa wateja kwa kuwa kufanya hivyo kutaboresha huduma zaidi.

Aliwataka watumishi kuwa na huduma zilizotukuka na kujenga uhusiano mzuri kazini kati yao. Kutasaidia kuboresha huduma kwa kiasi kikubwa.

Pia aliwataka kuachana na makundi kazini, mdogo kumheshimu mkubwa na mkubwa kumheshimu mdogo na kuacha dharau hata kama wana uhusiano wa kimapenzi.

"Ninatoa mfano, mtu mpenzi wako mganga mfawidhi au mkuu wa kitengo, unatakiwa ufanye kazi kwa weledi na si kudharau maagizo ya wengine unayopewa kwa kuwa wewe mpenzi wako ni bosi, hiyo sio sawa." alionya.

Alisisitiza tasnia ya afya haihitaji watu wazembe na wala haihitaji watu wenye roho mbaya.

"Weledi uanze getini kwa mlinzi, mapokezi hadi kwa kwa daktari husika. Mgonjwa anatakiwa afarijiwe kuanzia ngazi hizo na si kuwanyanyasa na kauli ambazo hazifai eneo la kazi," alionya.

Pia aliwataka madaktari wa wilaya na mikoa kujitayarisha katika majanga ya dharura katika vipindi vijavyo vya sikukuu za mwishoni mwa mwaka kwa kuwa kumekuwa na majanga mengi ambayo yamekuwa yakijitokeza.

Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufani Temeke, Dk. Josefu Kimaro alifafanua fedha walizopatiwa na serikali Sh. bilioni 4.9, wamezitumia kufunga mashine ya 'CT Scan' iliyogharimu zaidi ya bilioni mbili, kukarabati chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum (ICU) na kununua vifaa tiba mbalimbali.

Dk. Kimaro alisema mbali na fedha hizo ambazo walipewa mwaka jana, mwaka huu tayari wameshapokea Sh. bilioni tatu ambazo watazitumia katika kutoa huduma ya mama na mtoto kwa mujibu wa maelekezo kutoka Wizara ya Afya, na wamepokea Sh. milioni 600 kwa ajili ya kupanua hosptiali za wilaya.

"Tayari tushatoa mafunzo ya ubora kazini kwa watumishi wote 600 hospitalini hapa kutokana na agizo lililotolewa na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu.

"Fedha tulizopewa zimetusaidia kwa kiasi kikubwa sana kwani tumeweza kuboresha maeneo mengi hata hii CT Scan iliyofungwa ambayo ina muda wa miezi minne sasa, ina uwezo wa kuhudumia wagonjwa 150 kwa mwezi," alifafanua.

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Sixtus Mapunda, aliomba rukhsa kwa Naibu Waziri kuanza kwa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya eneo la Chamazi kwa kuwa fedha zimeshaingizwa lakini wanasubiri maelekezo.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Rufani Mwananyamala, Dk. Zavery Benela aliishukuru serikali kuwapatia Sh. bilioni 3.2 katika mradi ya UVIKO-19. Pia wamepatiwa fedha kwa ajili ya kufanya marekebisho katika jengo la ICU na kurekebisha mifumo ya oksijeni.

**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**DEO MWAKASINGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA LANDCRUISER yenye usajili namba T 827 AMD na CHASSIS NAMBA: JTEBE91JX00013257. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA : SOG/RB/4549/2023**

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**GS GROUP LIMITED** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **HAOJUE** yenye usajili namba **MC 393 DYE** na CHASSIS NAMBA: **LC6PCJK23P0022655.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA : **SOG/RB/4357/2023**

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**GS GROUP LIMITED** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **HAOJUE** yenye usajili namba **MC 373 DDW** na CHASSIS NAMBA: **LC6PCJK29M0A971195.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA : **SOG/RB/4550/2023**

**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**MERY HEPPIMAKI MKIRAMWENI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili T 944 DUU – SUBARU IMPREZA. Chassis namba GH2003016. Engina namba ELL5D146326.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/7523/2023.**

**KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI**

**RONALD YUDITHA MAZENGO** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya TV STAR yenye usajili namba MC 871 CKG na CHASSIS NAMBA: MD625AF42K1G09366. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA : **SOG/RB/5323/2023**

MADARASA YA NYASI

# Ukweli kuanikwa; DC, DED waamua kuyavunja

## ●Wajitetea ufumbuzi wake bajeti ya bilioni 18/-

**Na Mwandishi Wetu,**
aliyekuwa TUNDURU



Hali ya miundombinu na samani katika Shule ya Msingi Magomeni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

WIKI mbili baada ya mwandishi wa habari wa gazeti hili kuzungumza na uongozi wa Wilaya ya Tunduru kutaka kujua kwanini Shule ya Msingi Magomeni ina madarasa mawili yaliyojengwa kwa nguzo za miti na kuezekwa kwa nyasi, madarasa hayo sasa yamebomolewa.

Oktoba 27 mwaka huu, mwandishi wa habari hizi alifika katika shule hiyo na kukuta ina madarasa sita. Kati yake, mawili yamejengwa kwa hadhi hiyo ya nguzo za miti na nyasi.

Baada ya kushuhudia hali hiyo inayokinzana na miongozo ya kisera, ndipo Novemba 9 mwaka huu, akautafuta uongozi wa wilaya hiyo kuchimbua undani wa kinachojiri shuleni Magomeni.

Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Chiza Marando, wote wakatoa ufafanuzi kwamba madarasa ya nyasi yaliyoshuhudiwa shuleni huko "ni mahali panapotumiwa na wanafunzi kula chakula", lakini mwandishi alikuta kila darasa lina ubao wa kufundishia.

Hata hivyo, mwandishi aliporejea shuleni huko juzi (Novemba 19, 2023), alibaini madarasa hayo mawili ya nguzo za miti na paa la nyasi hayapo tena.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Magomeni, Ibrahim Kinyonga (76), alipoulizwa kuhusu kilichotokea, alisema madarasa hayo yalibomolewa siku sita zilizopita na Kamati ya Shule kwa amri ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru.

Si rahisi kugundua kwamba kulikuwa na madarasa ya miti isipokuwa mashimo ya nguzo na ubao wa kuandikia uliojengwa kwenye ukuta wa darasa lililojengwa kwa matofali ya saruji na kuezekwa kwa bati.

Shule hii yenye wanafunzi 183 (wasichana 89), ina vyumba vinne vya madarasa yaliyojengwa kwa matofali ya saruji na kuezekwa kwa mabati, ambayo yameanza kuota kutu.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti Kinyonga, madarasa mawili ya miti na nyasi yaliyobomolewa yalijengwa miaka minne iliyopita na wananchi wa Kijiji cha Magomeni kwa mpango wa kujitolea ili kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Marando, alipoulizwa juzi sababu za kubomoa madarasa hayo alisema, "ni kweli niliagiza yabomolewe kwa kuwa si madarasa yanayohitajika shuleni. Yalijengwa kwa ajili ya mahali pa kulia chakula shuleni."

Alisema madarasa hayo ya nguzo za miti na paa la nyasi, "yanatuletea image (sura) mbaya kwamba sisi Tunduru tuna madarasa ya nyasi. Kama kuna uhaba wa madarasa, hiyo ni issue (suala) nyingine."

Mwandishi pia alibaini Shule ya Msingi Nambalapi ina madarasa yaliyoezekwa kwa nyasi. Mkurugenzi Marando alitoa ufafanuzi kuwa yamejengwa na wananchi kwa mpango wa dharura baada ya shule hiyo kukumbwa na mafuriko Mei mwaka huu.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Magomeni (Kinyonga), anasema hajashirikishwa katika suala zima la kubomoa madarasa hayo na kwamba anashindwa kuelewa jinsi atakavyoeleza zoezi hili kwa wananchi.

"Hapa ninashindwa kuelewa watoto wa darasa la awali hadi la VII watavyosoma katika vyumba vinne vilivyobaki.

"Kwenye hayo madarasa ya nyasi walikuwa wanapishana, siku nyingine unakuta darasa la IV wanayatumia wakati mwingine la darasa la II, wengine wanakaa chini kwa sababu madawati ni machache," anasema.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Ezekiel Menge, alipotafutwa na mwandishi kuzungumzia hali ya miundombinu na samani shuleni, alisema walilazimika kutumia madarasa ya nyasi kufundisha wanafunzi kutokana na uhaba wa madarasa unaowakabili.

Katika vyumba vinne vya madarasa vilivyosalia, havitoshelezi wanafunzi 183 waliopo; sakafu imebomoka na mahali pengine pana mashimo: madawati ni machache na baadhi yamelegea kiasi kwamba mwanafunzi sharti ashikilie dawati lake wakati anaandika.

Plasta kwenye baadhi ya kuta imebanduka kiasi kwamba unaweza kuhesabu idadi ya matofali. Katika moja ya madarasa ubao wa kuandikia unaning'nia kiasi cha kudondoka wakati wowote.

Katika ofisi ya walimu ambako kuna meza mbili, kuna kiti kimoja tu (pichani) chenye 'miguu mitatu', mmoja umeshakatika.



Kinyonga anasema shule hii iliyosajiliwa mwaka 2002, ina walimu watano (wa kike wawili). Kati yao, watatu wanaishi katika nyumba tatu zilizoko shuleni (moja ilijengwa na wanakijiji miaka mitano iliyopita).

Anabainisha kuwa mwalimu mmoja anaishi katika nyumba ya kupanga kijijini Magomeni na mwingine (wa kiume) anaishi Kijiji jirani cha Majimaji, takriban kilometa nane kutoka shuleni Magomeni.

Kuhusu huduma ya choo, Kinyonga anabainisha kuwa Shule ya Msingi Magomeni ina matundu sita ya vyoo kwa ajili ya wanafunzi. Haina vyoo kwa ajili ya walimu wao. Wanatumia vyoo vilivyoko katika nyuma tatu za walimu.

Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, inaelekeza choo shuleni kitumike kwa uwiano wa 1:20, yaani tundu moja kwa wasichana 20 au 1:25 (tundu moja kwa wavulana 25). Pia kila shule ina na vyoo kwa ajili ya walimu wa kike na wa kiume.

Hivyo, kwa maelekezo hayo ya kisera, Shule ya Msingi Magomeni inapaswa kuwa na matundu manne kwa ajili ya wanafunzi wa kike 89 waliopo na manne mengine kwa ajili ya wanafunzi wa kiume 94 waliopo. Pia inapaswa kuwa na choo kwa ajili ya walimu wao.

Ibara ya 8(1)(d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) inaelekeza wananchi kushiriki katika shughuli za serikali yao. Wakazi wa Kijiji cha Magomeni wanashiriki kuinusuru shule yao?

Mwenyekiti Kinyonga anasema, "kwa sasa hali yetu si nzuri kiuchumi, msimu uliopita wa korosho haukuwa mzuri kwetu. Tuko tayari kutoa nguvukazi kama serikali italeta fedha za ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu."

Ado Shaibu, Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, anaitaka serikali iwajibike kuziondosha shule za nyasi wilayani Tunduru.

"Hali ya shule ya nyasi haikubaliki. Tunajua serikali inapambana kutatua changamoto za madarasa, madawati, walimu na vyoo katika sehemu mbalimbali ikiwamo Tunduru. Tunaunga mkono jitihada hizo. Lakini hili la kuwapo shule za nyasi Tunduru ni doa kubwa kwa serikali.

"Kwa kuanzia, Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru iwajibike kutumia mapato ya ndani. Mwaka juzi walikusanya Sh. milioni 700 na mwaka jana Sh. milioni 420 kutokana na tozo za mauzo ya korosho. Serikali inaweza kuanza kutumia fungu hili kuondosha shule za nyasi Tunduru," Shaibu anashauri.

**MIKAKATI SERIKALINI**

Unafuu pekee ambao Shule ya Msingi Magomeni inao, unatarajiwa kupatikana baada ya halmashauri kujenga vyumba viwili kutokana na mapato ya Sh. milioni 450 yatokanayo na mauzo ya korosho msimu huu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru (Marando), akizungumza hatua wanazochukua, alisema watajenga vyumba viwili vya madarasa katika shule hiyo mwaka huu wa fedha (2023/24) kwa kutumia mapato yao ya ndani.

Alisema wanahitaji Sh. bilioni 18 kukabili uhaba wa miundombinu na samani katika shule za msingi 153 za halmashauri hiyo.

Mkurugenzi Marando alisema serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya elimu wilayani Tunduru, ikiwapatia Sh. bilioni mbili mwaka 2022/23 na Sh. bilioni tatu mwaka huu wa fedha. Lakini hakuna fungu lililotengwa kwa ajili ya Shule ya Msingi Magomeni toka Serikali Kuu.

"Mwaka huu tutajenga madarasa mawili katika Shule ya Msingi Magomeni kutokana na mauzo ya korosho. Mnada wa kwanza wa korosho tayari umefanyika, tumepata tani 15,000. Hapo tuna uhakika wa halmashauri kupata Sh. milioni 450 (wanatoza Sh. 30 kwa kila kilo ya korosho)," alisema Marando.

Alisema kipaumbele ni kwa shule zenye idadi kubwa ya wanafunzi, akiitaja Shule ya Msingi Ligoma ambako sasa wanatekeleza mradi wenye thamani ya Sh. milioni 513.2. Wanajenga madarasa 14, matundu 24 ya vyoo, jengo la utawala na kichomea taka. Pia wanajenga madarasa ya mawili ya mfano elimu ya awali na matundu sita ya vyoo.

Mkurugenzi Marando pia alisema wanaendelea na ujenzi wa madarasa saba, matundu 14 ya vyoo, jengo la utawala na kichomea taka katika Shule ya Msingi Tinginya. Mradi huo ambao pia unajumuisha ujenzi wa mtundu sita ya vyoo na madarasa mawili ya mfano elimu ya awali, unagharimu Sh. milioni 331.6.

Kimsingi, kinachoshuhudiwa shuleni Magomeni, si tu kinakinzana na maelekezo ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, bali pia ni ishara ya kutofanyiwa kazi hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2017.

Katika ripoti yake ya Ukaguzi Maalum wa Miundombinu na Samani za Shule za Msingi Tanzania aliyoitoa Machi 2017, CAG (kipindi hicho, Prof. Mussa Assad) alibainisha hali mbaya ya miundombinu na uhaba wa samani na walimu katika shule zinazomilikiwa na serikali.

CAG alipendekeza serikali ichukue hatua za haraka kuboresha miundombinu iliyopo na kujenga mipya.

Wakati Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ikihitaji Sh. bilioni 18 kutatua changamoto ya uhaba wa miundombinu katika shule za msingi, uchambuzi wa Ripoti ya CAG kwa mwaka 2021/22 uliofanywa na Taasisi ya WAJIBU, umebaini Sh. bilioni 411.31 zimepotea katika mazingira yenye viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu katika matumizi ya kawaida, mishahara, mafao na rasilimali watu nchini kwa mwaka huo wa fedha.

Kiasi hicho kilichopotea, kama kingeelekezwa kutatua changamoto ya uhaba wa madarasa shuleni, kinatosha kujenga vyumba vya madarasa 20,565. Kwa mujibu wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, darasa moja linajengwa kwa Sh. milioni 20 likiwa na samani zake zote.

# Mikoa inayoongoza kukosa vyoo yatajwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MIKOA ya Katavi, Simiyu, Manyara, Tabora na Arusha imetajwa kuongoza kuwa na idadi kubwa ya watu wasiokuwa na vyoo.

Kadhalika, asilimia 9.8 ya watu nchini hawana vyoo kabisa na hali ni mbaya zaidi maeneo ya vijijini ambako asilimia 13.4 ya wakazi wanaojisaidia ovyo vichakani na maeneo mengine ambayo sio rasmi.

Taarifa ya hali ya uchumi iliyotolewa na Benki ya Dunia ya mwaka 2023 imeonesha Sh. trilioni 5.6 zinapotea kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo gharama za matibabu ya magonjwa, kutafuta maji na sehemu ya kujisaidia hasa kwa wasio na vyoo. Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, katika tamko la siku ya matumizi ya choo duniani alilolitoa juzi, alibainisha mikoa ambayo watu hawatumii choo na idadi kwenye mabano ni Katavi (24.3%), Simiyu (24.3%), Manyara (22.3%), Tabora (21.9%) na Arusha (20.5%).

Aliziagiza sekretarieti za mikoa na halmashauri kuhakikisha kaya zote nchini zinakuwa na vyoo bora.

Ripoti ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria ya mwaka 2022 imeonesha kuna ongezeko kubwa la watu wanao tumia vyoo bora kutoka asilimia 21 mwaka 2016 hadi asilimia 74.8 mwaka 2022.

"Licha ya kupiga hatua kwenye kiashiria hicho, bado kuna baadhi ya watu hawatumii vyoo, takwimu zinaonesha kuwa asilimia 9.8 ya watu nchini hawana vyoo kabisa ambapo hali ni mbaya zaidi maeneo ya vijijini. Kwa mujibu wa taarifa hii asilimia 13.4 ya wakazi wa vijijini hawana vyoo kabisa. Tafsiri ya kiashiria hiki ni kwamba watu hawa ndiyo wanaojisaidia ovyo vichakani na maeneo mengine ambayo sio rasmi," alisema.

Alisema hali hiyo inachangia kuwapo kwa magonjwa ya mlipuko ikiwamo kipindupindu na kwa kipindi cha Januari hadi Oktoba, 2023 watu 749 waliougua na16 kupoteza maisha.

Kadhalika, ripoti hiyo inaonesha bado kuna asilimia 30 ya udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano ambayo inachangiwa na kukosekana kwa vyoo bora kusababisha magonjwa ya kuhara na mwili kupoteza virutubisho.

Alitoa rai kwa jamii kuendelea kuboresha vyoo vyao kuwa kwenye hali ya ubora.

"Kutokana na tahadhari ya kuwapo kwa mvua kubwa ya Elnino, niikumbushe jamii kuwa na miundombinu imara ya vyoo ili kuhimili mvua inayotarajiwa kunyesha ili kuepukana na hali hii ni vyema vyoo vikaboreshwa kwa kujenga mashimo imara," alisema.

Waziri Ummy alisema katika kuendelea kuwezesha jamii kujenga na kutumia vyoo bora, mikoa na halmashauri ifanye ukaguzi kwenye kaya, sehemu za jumuiya, maeneo ya biashara na taasisi zote kwa kujenga na kutumia vyoo bora.

"Pia wahakikishe wanasimamia vyema Sheria ya Afya ya Jamii na Sheria Ndogo zinahusiana na ujenzi na matumizi ya choo bora kwenye ngazi ya kaya, taasisi na maeneo ya jumuiya," alisema.

Alisisitiza zisimamie vyema matumizi ya vyoo kwa wasafiri wawapo safarini kwa kuhakikisha mabasi yanasimama kwenye maeneo rasmi ikiwamo stendi za mabasi na vituo maalum.

"Ni marufuku tabia ya wasafiri kujisaidia ovyo maarufu kama kuchimba dawa. Ni aibu kwa taifa na pia udhalilishaji wa utu," alisema.

# Masauni 'tuzingatie ubinadamu'

**Na Halfani Chusi**

SERIKALI imewataka Watanzania kuishi kwa kuzingatia thamani za kibinadamu zinazojumuisha huruma, uvumilivu, umoja, na juhudi za maendeleo ya binadamu, kulingana na mafundisho ya nabii.

Rai hiyo alitolewa juzi na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, katika hafla ya kusherehekea siku ya kuzaliwa kwa Mtume Muhammad iliyo andaliwa na Jumuiya ya Ismaili.

Aliitaka jumuiya hiyo inayomiliki Hospitali za Aga Khan kuangalia uwezekano wa kupunguza gharama za matibabu ili Watanzania wenye kipato cha chini waweze kumudu gharama.

Masauni alisema baada ya kutoa ombi hilo liliitikiwa kwa shangwe na ana uhakika litafanyiwa kazi kwa kuwa limetoka kwa mkuu wa nchi.

"Nina wapongeza sana Jumuiya ya Ismaili kwa kuadhimisha kuzaliwa kwa Mtume Muhammad, lakini nimeona mchanganyiko wa madhehebu mbalimbali hii inaashiria kwa vitendo ile sera ya umoja, mshikamano na upendo baina ya Watanzania wenye imani tofauti, kabila na asili.

"Tunatambua kazi nzuri wanazozifanya kwa kutoa mchango mkubwa katika sekta ya afya, elimu, uchumi, ninyi ni mashahidi juu ya huduma nzuri ya afya zinazotolewa na hospitali mfano ile ya Aga Khan inasifika kwa huduma nzuri."

Mwakilishi wa Kidiplomasia wa Aga Khan Development Network nchini (AKDN), Amin Kurji, alisema watalifanyia kazi ombi la serikali la kushusha gharama za matibabu, huku akiwasisitiza Watanzania kuitikia wito wa serikali wa bima ya afya kwa wote.

Alisema ili uweze kupata matibabu mazuri, lazima uwe na bima ya afya, itakayosaidia kumudu gharama za matibabu na mpango wa bima ya afya kwa wote utawasaidia Watanzania wengi kupata matibabu bora yenye gharama za juu.

"Na si tu kwa hospitali za Aga Khan, bali hata kwa zahanati nyingine, lakini kuhusu ombi la serikali tutaangalia, vituo vyetu vya afya vipo 36 nchi nzima. Hii ya Aga Khan ni kama ya rufani, lazima upitie huko halafu ndio wakulete hapa.Kwahiyo, tutaona nini cha kufanya," alisema.

# TEA yajenga zaidi ya madarasa 300 kipindi cha Samia

**Na Gwamaka Alipipi**

MAMLAKA ya Elimu Tanzania (TEA), imesema katika kipindi cha uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan imejenga madarasa 376 kwa Sh. bilioni 58, pamoja na kukarabati shule kongwe 11 kwa Sh. bilioni 20.

Kaimu Mkurugenzi Utafutaji Rasilimali na Miradi wa mamlaka hiyo, Masozi Nyirenda, alitoa taarifa hiyo jana jijini Dar es Salaam kwa waandishi wa habari wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya TEA.

Nyirenda alisema kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa unaoratibiwa na TEA, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Sh. bilioni 10.99 ziligharamia ufadhili wa miradi 132 ya kuboresha miundombinu ya elimu katika shule 151 nchini.

Alitaja miradi hiyo kuwa ni ujenzi wa vyumba 114 vya madarasa katika shule 38 zikiwamo shule mbili za sekondari na 36 za msingi.

"Mradi unatarajiwa kunufaisha wanafunzi wapatao 6,840, Sh. bilioni 3.3 kinatumika. Madarasa 85 yamekamilika, 30 yako katika hatua za mwisho na tisa yapo hatua za kati," alisema Nyirenda.

Alitaja mradi mwingine ni ujenzi wa maabara 10 za sayansi katika shule tano za sekondari, kwamba unatarajiwa kunufaisha wanafunzi 450, thamani ya miradi hiyo ni Sh. milioni 590.5.

Nyirenda alisema kupitia ufadhili wa serikali wamefanikiwa kujenga nyumba 52 za walimu katika shule 13, shule saba zikiwa za msingi na shule sita zikiwa za sekondari.

Alisema mradi huo unatarajiwa kunufaisha walimu 52 pamoja na familia zao, thamani ya miradi hiyo ni Sh. bilioni 2.7.

Kadhalika, alisema wamewezeka kujenga matundu 888 ya vyoo katika shule 37 zikiwamo shule 29 za msingi na shule nane za sekondari.

"Mradi huu unatarajiwa kunufaisha wanafunzi 21,312. Thamani ya miradi hii ni Sh. bilioni 2.06. Jumla ya matundu 120 yamekamilika, 600 yamo katika hatua za kukamilishwa na 168 yapo hatua ya kati," alisema Nyirenda.

Alisema pia wamejenga miundombinu kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule nane, shule saba za msingi na moja ya sekondari.

Vile vile, wamejenga madarasa 10, matundu ya vyoo 50 na mabweni matatu, kwamba mradi unatarajiwa kunufaisha wanafunzi wenye mahitaji maalum 2,010. Alisema thamani ya miradi hiyo ni Sh. milioni 609.3.

Aidha, wamejenga mabweni ya wasichana katika shule 12 za sekondari, kwamba mradi huo unatarajiwa kunufaisha wanafunzi wakike 1,440 na wa kiume 120.

Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Dk. Erasmus Kipesha, alisema kuanzia mwaka 2018 hadi mwaka huu ruzuku ya Sh.bilioni 20.19 zimetumika kufadhili mafunzo kwa wanufaika 49,060.

Alisema kati ya idadi hiyo wanawake ni 22,410 (46%) na wanaume 26,650 (54%) ambao wamepata mafunzo ya ujuzi katika sekta ya kilimo na kilimo Uchumi, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, utalii na huduma za ukarimu, nishati, ujenzi na uchukuzi.

Alisema vijana walionufaika na mfuko huo ni 464 waliotoka kundi la wenye ulemavu, 2,928 walitoka kundi la vijana kutoka kaya masikini na wanaoishi katika mazingira magumu kwa Tanzania Bara, 600 walitoka kaya masikini na wanaoishi katika mazingira magumu kwa upande wa Zanzibar.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
21.11.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Jumamosi tarehe 25-11-2023 hadi 30-11-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Holili Border** kuelekea **Kilombero kupitia Babati, Dodoma,** gari hizo zina namba za usajili: **T 453 DYG /T 837 DJB T 853 DXS / T 887 DJB**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 25.00**
**Upana - mita 4.80**
**Kimo - mita 5.40**

3. Njia itakayotumika: **Moshi, Arusha, Manyara, Dodoma, Morogoro hadi Kilombero kupitia Mikumi,** gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
21.11.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Alhamisi tarehe 23-11-2023 hadi 26-11-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port kuelekea Kilombero** kupitia Mikumi, gari hizo zina namba za usajili: **T 957 DTN /T 877 EAU, T 308 EDD /T 630 AJA**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 23.00**
**Upana - mita 4.40**
**Kimo - mita 5.40**

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero kupitia Mikumi,** gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waliozingirwa na mafuriko ya mvua wasaidiwe

**TANGU** mvua kubwa iliyonyesha Novemba 12 na kusababisha maafa ya kukumbwa na mafuriko, bado wanaoishi katika maeneo hayo wanapata shida baada ya maji kukosa njia ya kutokea.

Kwa mfano wakazi wanaoishi eneo la Boko Basihaya, Barabara ya Bagamoyo wako katika shaka kubwa kutokana na maji ya mafuriko kuendelea kuzingira eneo hilo kwa kukosa njia ya kutokea.

Kila mara eneo hilo hukumbwa na mafuriko inaponyesha mvua kubwa na madhara yake yanaonekana, lakini bado hakuna hatua zinazochukuliwa kuondoa tatizo hilo.

Viongozi kadhaa wameshatembelea eneo hilo na kutoa ahadi za kuondoa kero hiyo, lakini mpaka sasa hakuna kinachoendelea.

Baadhi ya wakazi hao ambao nyumba zao zimezingirwa na maji wamepata hasara kubwa ya kuharibikiwa na mali baada ya maji hayo kuingia ndani na nyumba zingine maji kufika karibu na paa za nyumba.

Kwa wale wenye uwezo, wamelazimika kuziacha nyumba zao na kwenda kutafuta viwanja maeneo mengine na kujenga. Kwa wale ambao hawana uwezo huo wanaendelea kuteseka kila mvua kubwa inaponyesha na kusababisha mafuriko.

Kwa wanaopita Barabara ya Bagamoyo eneo hilo la Basihaya, watashuhudia baadhi ya nyumba ambazo ziko karibu na barabara zikiwa zimezingirwa na maji ambayo sasa ni wiki moja imepita toka mvua kubwa iliponyesha.

Maji hayo sasa yameanza kubadilika rangi na kuwa ya kijani kutokana na uchafu uliosombwa na mafuriko hayo.

Hii ni hatari kwa wakazi wa eneo hilo kwasababu yatakuwa mazalia ya mbu wanaosababisha ugonjwa wa malaria na vile vile ni hatari kwa watoto wanaocheza maeneo hayo.

Watoto wengine wanachezea maji hayo kwa kuogelea jambo ambalo pia ni hatari kwa sababu wanaweza kupata magonjwa ya njia ya mkojo na kichocho.

Tatizo kubwa la eneo hilo kujaa maji ni kukosa mifereji ya kusafirishia maji hayo na kalavati kubwa lenye uwezo wa kupitisha maji hayo kwenda baharini.

Wanaoishi eneo hilo ni binadamu ambao wanahitaji kuangaliwa ili waondokane na tatizo hilo na adha ya kila mara kukumbwa na mafuriko.

Kwa sasa kama bajeti ya kuchimba mifereji haijatengwa ni bora hata ukafanyika utaratibu wa kuyanyonya maji hayo na kuondoa bwawa hilo.

Maji hayo yakiachwa kwa muda mrefu tunaweza kushuhudia samaki aina ya kambale wakivuliwa sehemu hiyo.

Kuna watu wanaofanya biashara eneo hilo, lakini maji yaliyojaa yanawakwamisha kuendelea na shughuli zao ambazo ndizo wanazotegemea kuwaingizia kipato.

Biashara zimefungwa na wengine wana mikopo ambayo imewasaidia kwenye mitaji ya kuanzisha biashara hizo na wanatakiwa kuirudisha, lakini kutokana na kukwama kufanya shughuli zao wanashindwa na deni linazidi kuongezeka.

Familia zinawategemea kwa kila kitu, katika hali hii unakuta baadhi ya watu wakitembea barabarani wanaongea wenyewe kama waliorukwa na akili.

Ni vyema juhudi zikafanywa ili maji hayo yakaondolewa mara moja na kuwaacha watu waishi kwa usalama.

Walioathirika na maji ya mvua sio wa mabondeni pekee kwa sababu mvua hiyo ilikuwa kubwa na kuleta athari ya kubomoa miundombinu na kusababisha maji kusambaa na kuharibu nyumba na barabara.

Umakini pia unahitajika katika kubaini maeneo mtu anapohitaji kujenga makazi sehemu yenye usalama.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Pamoja tuwarejeshe waliokacha shule

**WITO** wa kuita wadau kufanya utafiti wa mpango wa kurejesha shuleni wasichana waliokatisha masomo kwa sababu mbalimbali umesikiwa na sasa wahusika kazi kwetu.

Ni ombi la serikali ambalo linapaswa kuungwa mkono na wazazi, walezi na jamii ili kuleta mafanikio na kutimiza ndoto za mabinti hao ili wamalize masomo na kulitumikia taifa sasa na baadaye.

Serikali inachukua uamuzi huo kubaini mafanikio na vikwazo vinavyowakabili hadi kuacha masomo, ikilenga kupata mapendekezo ya kumpa kila mtoto nafasi kielimu.

Katika kutekeleza Waraka wa Elimu namba 3 wa mwaka 2021 wa kuwarejesha shuleni wasichana waliokatisha masomo hadi sasa ni 7,995 waliorejeshwa madarasani, inasema Wizara ya Elimu.

Wanaendelea na masomo kupitia mfumo rasmi na usio rasmi wa elimu, hatua ambayo serikali inastahili pongezi pamoja na wazazi na walezi kwa ushirikiano kilichofikisha kuvuka kiwango hicho.

Baada ya serikali kutoa tangazo, wana jamii na familia tunatakiwa kuwa bega kwa bega kwa sababu tunawafamu na tunaishi nao mitaani, tena tunashuhudia nyendo zao.

Kama kila mmoja akishiriki kufanikisha mpango huo wa serikali kuwarejesha watoto shuleni, ni dhahiri tutaokoa wengi badala ya kuwaacha wakizagaa mitaani na kujihusisha na uhalifu.

Jamii imekuwa ikishuhudia watoto wengi wakiwamo wa kike ambao wameacha shule kutokana na ujauzito, uvutaji bangi na utoro wakizagaa mitaani bila ya kuwa na shughuli maalumu.

Watoto hao kwa mfano wa kike wamekuwa wakishiriki katika biashara za ngono, vilabu vya pombe za kienyeji, baa na kuchezesha michezo ya kamari maarufu kubeti au 'glugluglu' angalau walipwe ujira ili kujikimu kimaisha na familia zao.

Wengi wao wamejikuta wakijiingiza katika ulevi wa kupindukia wa pombe kali ambazo zimekiuzwa kwa bei ya chini kuanzia asubuhi, wakidai wanapoteza mawazo kutokana na hali ngumu ya maisha mitaani bila kujua kama wanapoteza mwelekeo wa maisha.

Ni dhamira nzuri ya serikali kufanya tathmini hiyo kwa sababu itawabaini wazazi na walezi ambao wamekuwa wakinufaika na watoto wa kike walioacha masomo kwa ujauzito.

Inawezekana wapo ambao wanawatumia kupata fedha kwa baba zao huku wengine wakitumia mwanya huo kuwaoza kama njia ya kukabiliana na ukata kwa kulipwa mahari ya fedha na mifugo.

Pia mwito huo ni kuona mafanikio na changamoto walizonazo ili kuangalia namna bora zaidi ya kutekeleza maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Katika kufanikisha hilo, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) kwa mujibu wa Waziri wa Elimu, Profesa Adolf Mkenda, linashirikiana na wizara yake kutoa fedha za utafiti kwa kufuatilia wote ambao wamerudi shule mmoja mmoja kumhoji.

Aidha, kuangalia mazingira, mafanikio, changamoto na mapendekezo ya namna bora zaidi ya kutekeleza maelekezo ya Rais Samia ya kuhakikisha kuwa hakuna mtoto atakayeachwa nyuma kwenye elimu.

Mkenda anasema watoto wengi wanaocha shule ni wa kiume, lakini angependa utafiti huo uanze kwa awamu ya kwanza kufuatilia wa kike waliorudi shuleni.

Anakumbusha kuwa serikali imejenga shule mpya 26 za wasichana kwa kila mkoa kwa Tanzania Bara na moja kila kata kwa watoto wa kike na wa kiume na kupunguza umbali kutoka nyumbani kwenda shuleni na kuondoa changamoto ambazo wangekutana nazo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, Husna Sekiboko, anasema bunge na kamati haitakuwa kikwazo katika mipango ya serikali ya kumwendeleza na kumlinda mtoto wa kike nchini.

Mwakilishi wa UNICEF, Dk. Daniel Baheta, anasema shirika hilo litaendelea kujitolea kuunga mkono jitihada za serikali kuwaendeleza wasichana na kuwawezesha huku akipongeza uamuzi wa kuruhusu watoto wa kike waliopata ujauzito kurudi shule kuendelea na masomo.

Hivyo kama wazazi na walezi wana kila sababu ya kumpongeza Rais Samia na kumuunga mkono kwa kusaidia kuwafichua wanafunzi zaidi ili warudishwe shuleni.

HABARI KITAIFA



Wakazi wa Bunju na maeneo jirani wakisubiria huduma za afya katika kambi maalum iliyoandaliwa na klabu za Rotary Dar es Salaam na Bahari katika Shule ya Msingi Bunju A mwishoni mwa wiki. Zaidi ya wananchi 1,000 walipatiwa vipimo, matibabu na ushauri wa bure wa afya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mvua yasababisha vifo vya watu wawili

**Na Jaliwason Jasson,** MBULU

MKUU wa Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara, Kheri James, amesema mvua inayoendelea kunyesha imesababisha vifo vya watu wawili katika Mgodi wa Saraa.

Kutokana na mafuriko katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo, James ameshauri wananchi kuachana na safari zisizokuwa za lazima ili kuepuka madhara ya mvua.

Ni rai aliyoitoa alipozungumza na wananchi wa wilaya hiyo katika Shule ya Sekondari Nowu juzi, akibainisha kuwa barabara na maeneo ya huduma yameanza kuharibika kutokana na mvua.

Aliwaomba wazazi wakiona watoto wamechelewa kutoka shuleni, wawafuate au wafuatilie wanaweza wakawa wamecheleweshwa na mvua au imewaathiri njiani. "Niwatoe wasiwasi kuwa barabara zikipata shida tutazitafutia ufumbuzi wa haraka. Cha msingi mtupe taarifa mapema ili Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) waweze kuzifanyia kazi," alisema James.

Vilevile, Mkuu wa Wilaya alitaka wananchi kuitumia vizuri mvua hiyo kufanya shughuli za kilimo ili kuepuka baa la njaa na likitokea wao wawe sehemu ya kusaidia wenye njaa.

"Mbulu ninajua ninyi siyo ombaomba, ni wachapakazi. Ninajua mtaitumia vizuri mvua ili mjiongezee kipato," alisema.

Alitumia fursa hiyo kuwasisitiza wazazi kuzijengea msingi mzuri familia akiwa na hoja kwamba zikilegea, kila kitu kinalegea na viongozi watapata shida kuwaongoza watu wenye familia legelege.

Mkuu wa Wilaya alisema familia zikilelewa vizuri, viongozi wa serikali wanarahisishiwa kuziongoza kwa kuwa ulevi, wizi au unyang'anyi unaanzia ngazi ya familia.

# TBS yatoa leseni kwa wajasiriamali

**Na Joseph Mwendapole**

WAJASIRIAMALI 145 wamepatiwa vyeti na leseni na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) baada ya bidhaa zao kuthibitishwa na kukidhi matakwa ya viwango kwa kipindi cha kuanzia Juni hadi Novemba mwaka huu.

Hafla ya kukabidhi vyeti na leseni kwa wajasiriamali hao ilifanyika mwishoni mwa wiki iliyopita kwenye ofisi ya Makao Mkuu ya TBS, mkoani Dar es Salaam.

Kaimu Mkurugenzi wa TBS, Lazaro Msasalaga, alisema vyeti na leseni hizo ni uthibitisho kuwa wazalishaji nchini wanao uwezo mkubwa wa kuzalisha bidhaa ambazo zina uwezo wa kushindana katika soko la ndani na la nje.

Alibainisha kuwa kwa kipindi hicho cha Juni hadi Novemba mwaka huu, vyeti na leseni ambazo zimetolewa ni 145. Kati yake, vyeti vya ubora wa mifumo ni sita.

Msasalaga alibainisha kuwa vyeti na leseni kwa wazalishaji ambao tayari walikuwa na leseni ya TBS, lakini walikuwa wanazalisha bidhaa mbili zinazofanana na sasa wameamua kuongeza bidhaa nyingine, ni 13.

Aliendelea kufafanua kuwa vyeti na leseni 60 kati ya hivyo 145 sawa na asilimia 43 ya vyeti vyote vilivyotolewa ni kwa wajasiriamali wadogo.

Msasalaga alisema anapotoa takwimu za wazalishaji wadogo (wajasiriamali) maana yake ni kwamba serikali inatoa huduma za uthibitishaji ubora wa bidhaa za wajasiriamali wadogo na kwamba yenyewe ndiyo inalipia gharama hizo.

"Maana yake vyeti hivi 60 kati ya 145 ambavyo vimetolewa kwa wajasiriamali wadogo watakuwa mashahidi kwamba walichokuwa wanatakiwa kufanya wao ni utambulisho kutoka SIDO kwamba wamekidhi matakwa ya viwango na hivyo wako tayari kupata huduma TBS," alisema.

Kiongozi huyo alisema huo ni ujumbe kwa wazalishaji kuwa ubora wa bidhaa unatoa ushindani mkubwa kwa wazalishaji bidhaa kama zao, hivyo watakuwa na uhakika wa soko.

"Ubora huu ni matakwa ya sheria, kanuni na miongozo ya hiari kwa wazalishaji bidhaa ili kuhakikisha watumiaji wanapata bidhaa bora muda wote, walaji au watumiaji wa bidhaa zetu wanapenda kuhakikisha wanapata bidhaa bora muda wote," alisema Msasalaga.

Aliongeza kwamba anasisitiza hilo kwa sababu wakati mwingine wazalishaji wanajisahau, wanafanya vizuri kwa sababu wanataka kupata nembo ya TBS , lakini baadaye wanarudi kwenye uzalishaji usiozingatia matakwa ya viwango.

"Hivyo, wazalishaji tuondoke na ujumbe huu ili kuhakikisha tuzalisha bihaa bora zinazokidhi matakwa ya viwango ili kulinda afya za walaji na masoko yetu kwa namna ambayo ni endelevu," alisisitiza Msasalaga.

Alisema wanapothibitisha bidhaa na kutoa leseni na vyeti, maana yake wateja wao watapata imani zaidi kuhusu ubora na usalama wa hizo bidhaa kwa sababu lengo la kuzalisha ni kuweza kuuza na kukuza bishara.

"Kwahiyo, kwa kuthibitisha bidhaa hizi tunawaongezea imani walaji wetu, hivyo kuongeza tija katika shughuli zetu za uzalishaji na kwa kuwa imani ya walaji inaongezeka watu wengi watazinunua bidhaa hizo na zitapata faida ya kiushindani.

"Jambo kubwa zaidi ambalo wengi wenye vyeti hivi vya ubora wamefanikiwa ni kwamba katika soko hilo la Afrika Mashariki, tumeshawianisha mifumo, tumeshawianisha masuala ya mifumo ya uthibiti ubora, tumewianisha viwango vya bidhaa mbalimbali," alisema.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Holcim Group yakubali kuuza Mbeya Cement

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya saruji ya Holcim Group ya Uswisi, imetangaza mpango wa kuuza kampuni yake tanzu Pan African Cement, ambayo inamiliki asilimia 65 ya hisa katika Kampuni ya Saruji Mbeya kwa Kampuni ya Amsons Group.

Hatua hiyo inaifanya Holcim kujiondoa katika soko la saruji Tanzania, kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa mwishoni mwa wiki ikiwa ni sehemu ya mkakati wake kuelekea mwaka 2025 wa 'Kuharakisha Ukuaji wa Kijani' ambao unalenga katika kuimarisha uongozi wake katika masoko ya msingi.

"Kampuni ya Holcim Group imefikia makubaliano na Kampuni ya Amsons Industries (T) Ltd ya kuiuzia kampuni yake tanzu ya Pan African Cement Limited ambayo ina hisa asilimia 65 katika kampuni ya Mbeya Cement," alisema Ofisa Mtendaji Mkuu wa Holcim's Lafarge Tanzania, Medhat Ismail, katika taarifa hiyo.

Ismail aliongeza katika taarifa hiyo kuwa mchakato wa kuuza kampuni hiyo tanzu ya Pan African Cement kwenda Kampuni ya Amsons Group, uko katika hatua ya kuidhinishwa na mamlaka husika za serikali.

"Tumefurahi kupata mshirika wa kimkakati na anayeaminika wa biashara huko Amsons Group, ambayo iko katika nafasi nzuri ya kuendelea kuwekeza katika ukuaji wake wa muda mrefu," aliongeza Ismail.

Hadi kukamilika kwa mkataba huo wa kuuza hisa zake kwa dola za Kimarekani milioni 160 (Sh. Bilioni 424) taarifa hiyo ilisema shughuli za kampuni ya Mbeya Cement zitaendelea bila usumbufu na kudumisha kasi na viwango vya biashara.

"Holcim inasisitiza ahadi yake kwa wafanyakazi wake wa Mbeya Cement, tunatambua na kuathmaini mchango wao katika ukuaji wa kampuni. Kampuni inathamini kujitolea kwa mnunuzi katika kukuza talanta za ndani na kukuza utamaduni unaohimiza ukuaji na maendeleo," alisema.

Holcim imeyaelezea makubaliano ya kuuza kampuni yake na Amsons Group kama hatua nzuri kwa wadau wote wanaohusika.

"Hatua hii inaashiria fursa ya matumaini kwa mustakabali mzuri na wenye faida kwa Mbeya Cement kuhakikisha mwendelezo na ukuaji wa biashara," alisema Ismail.

Hivi sasa, Amsons Group ina ushiriki mkubwa katika sekta za mafuta na gesi na bidhaa zilizosindikwa kwa watumiaji katika nchi za Tanzania, Msumbiji na Zambia.




Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (katikati), akisikiliza maelezo ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya maji Dar es Salaam kutoka kwa Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Kiula Kingu, katika hafla ya utiaji saini mkataba wa mradi na Kampuni ya M/S SINOHYDRO ya China. Kulia ni Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Uwekezaji Ziwa Victoria kuinua Bandari ya Dar

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema itatumia vyema fursa ya kijiografia kuvutia na kuimarisha uwekezaji katika Ziwa Victoria ambao utasaidia kuimarisha Bandari ya Dar es Salaam.

Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi, Profesa Godius Kahyarara, alisema hayo wakati wa hafla ya uzinduzi wa meli kubwa ya New MV Umoja Kazi Iendelee na utiaji saini mikataba ya ukarabati wa meli tatu hafla iliyofanyika katika Bandari ya Mwanza South.

Meli hiyo ina uwezo wa kubeba treni yenye mabehewa 22 itakayokuwa inafanyakazi kati ya Mwanza na Uganda, ambayo itawezesha wafanyabiashara kusafirisha bidhaa zao kwa urahisi na haraka zaidi.

Alisema serikali imedhamiria kufanya uwekezaji mkubwa katika Ziwa Victoria kwa lengo la kuimarisha Bandari ya Dar es Salaam, kuinua uchumi wa Kanda ya Ziwa na Tanzania kwa ujumla.

"Huu uwekezaji ni matokeo ya utekelezaji wa maelekezo ya Rais Samia aliyoyatoa bungeni Aprili 22, mwaka 202. Uwekezaji mkubwa ambao umefanyika ni pamoja na kukamilisha ukarabati wa meli ya MV. Umoja Kazi Iendelee," alisema Profesa Kahyarara.

Alisema ukarabati huo umegharimu zaidi ya Sh. bilioni 19.8 uliokwenda sambamba na mradi mkubwa wa ujenzi wa meli ya mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 3,500 katika Ziwa Tanganyika.

Pia meli ya mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 3,000 katika Ziwa Victoria na kwamba miradi hiyo imetengewa zaidi ya Sh. bilioni 625.

Aidha, hafla hiyo ilishuhudia utiaji saini wa mikataba mitatu ya ukarabati wa meli ya mafuta ya MT. Nyangumi yenye uwezo wa kubeba lita 400,000 za mafuta, meli ya uokozi ya MT. Ukerewe na meli kongwe ya abiria ya MV. Liemba iliyopo Ziwa Tanganyika.

Kwa mujibu wa Profesa Kahyarara, uwekezaji huo utaiwezesha Tanzania kunufaika na fursa ya kijiografia, uhusiano mzuri na fursa ya utulivu wa kisiasa pamoja na diplomasia ya kiuchumi kwa kuwa Bandari ya Dar es Salaam itakuwa na uwezo wa kuhudumia nchi zote za Maziwa Makuu.

"Uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya reli utawezesha kuunganisha reli za nchi jirani kupitia maalum kwa kubeba treni kama hii MV Umoja kwa hivi sasa zaidi ya asilimia 80 ya shehena ya nchi jirani inakwenda nchi za kusini na hata nchi yenye shehena kubwa ya Uganda inapitisha chini ya asilimia mbili pekee kupitia Ziwa Victoria.

"Lengo ni kuhudumia nchi zote za maziwa makuu mpaka Sudan ya Kusini Somalia na nyinginezo zitakazoona fursa hii inafaa, tunaamini hili linawezekana ndiyo maana serikali imeweka nguvu nyingi kwenye uwekezaji huu," alifafanua.

Profesa Kahyarara alisema faida za kiuchumi ni kubwa kwa nchi kwa kuwa kutakuwa na ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja, huku nchi ikiongeza wigo wa kuhudumia nchi zisizo na bahari.

# Wanaosoma usimamizi wa bima kufadhiliwa

**Na Valency Mbaga,** TUDARCo

KAMPUNI ya Bima la Britam imeahidi kutoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi katika mwaka ujao wa masomo.

Mwenyekiti wa Bodi wa Kampuni hiyo, Dk. Kuria Muchiru, alitangaza neema hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa shehere ya maadhimisho ya miaka 25 ya kampuni hiyo iliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Ikianzishwa mwaka 1998 na wafanyakazi watano, Kampuni ya Bima ya Britam Tanzania ikawa kampuni ya pili ya bima iliyosajiliwa nchini.

Tangu wakati huo imekua na kujiweka kama mtoaji wa suluhisho la ubunifu na la kina la bima ikijumuisha bima ya magari, afya, usafiri na uhandisi.

Katika maadhimisho hayo, kampuni hiyo ilizindua mpango wa ufadhili wa masomo uliopewa jina la 'Britam Scholarship' ambao kwa kuanzia, utatoa msaada wa kifedha kwa wanafunzi wawili wanaoendelea na masomo ya Bima na Usimamizi wa Vihatarishi.

Muchiru alisema mpango wa ufadhili wa masomo ni ishara ya shukrani na kukuza uwajibikaji wa kijamii kwa lengo la kuboresha ustawi wa watu wa Tanzania.

Vilevile alieleza shirika hilo linaendelea kufanya kazi zake kwa juhudi na uaminifu mkubwa kama kaulimbiu yao ili kuzidi kujenga uaminifu kwa wazawa na kuwa shirika bora zaidi kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Farai Dogo, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Britam Tanzania, alisema wameweka kipaumbele katika uvumbuzi wa bidhaa, athari kwa jamii, kuridhika kwa wateja na uongozi wa sekta katika azma yake ya kuwapa wateja wake uzoefu.

"Miaka 25 iliyopita tulipata sana changamoto ya wafanyakazi, mtaji na hatukuwa na watu wa ndani ambao walituamini na kuwekeza nasi na hivyo ilitubidi kutafuta wawekezaji wa nje ili kusaidia kutatua changamoto hizo.

"Pia kuna wakati hapa nchini palikuwa na mashirika matatu tu yanayohusika na utoaji wa bima, hivyo miaka ile hali ilikuwa si nzuri kabisa," alisema Dk. Lyzer.

Mgeni rasmi katika hafla hiyom, Kamishna wa Bima, Dk. Bakayo Zakware, alisema anatambua kazi na mchango mkubwa wa kampuni hiyo kwa serikali na jamii ikiwamo kulinda maisha ya watu, mali, afya na kuhimiza maendeleo hasa kupitia sekta binafsi ili kuchochea maendeleo ya nchi.

"Ninatambua jitihada zinazofanywa na serikali hasa kiongozi wetu wa nchi Rais Samia Suluhu ili kuhakikisha sekta ya bima nchini inakua kama inavyopaswa.

Aliwataka kuendelea kuboresha huduma zao ili kutoa huduma bora zaidi ikiwa ni pamoja na kujenga soko lenye taaluma, tija, kuvutia uvumbuzi wa teknolojia na kujiepusha na ulaghai,

Katika hafla hiyo, mgeni rasmi alikabidhi tuzo za heshima kwa watumishi waliotumikia kampuni hiyo kwa muda mrefu.

# TANAPA yapewa jukumu kuunganisha watalii Zanzibar na Hifadhi ya Mkomazi

**Na Godfrey Mushi,** SAME

SERIKALI imelitwisha jukumu zito la ushawishi, Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), kuhakikisha makundi makubwa ya watalii wanaoshuka Zanzibar, hawaondoki nchini bila kwenda kuwaona faru weusi na wanyama wengine wakubwa watano walioko Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi.

Utalii wa faru weusi katika hifadhi hiyo, umeongeza idadi ya watalii kwa asilimia 100, kati ya mwaka wa fedha 2021/2022, ukilinganisha na miaka mingine iliyopita.

Jana, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Dastan Kitandula, akiwa katika Hifadhi ya Taifa Mkomazi, Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, alisema TANAPA inapaswa kuiunganisha hifadhi hiyo na utalii wa Zanzibar ili kuongeza idadi ya watalii wanaoitembelea.

"Hakuna haja ya kuachia makundi makubwa ya watalii wanaozuru Zanzibar kuondoka, wakati mmeboresha viwanja vya ndege. Ni wajibu wa TANAPA kutumia fursa na mikakati ya kuwashawishi watalii kutoka Zanzibar kuja kuwaona Faru na wale wanyama wakubwa watano.

Alisema hifadhi hiyo ina sifa ya kuwa na faru adimu ambao kama wakifanikiwa kuwashawishi watalii kutoka Bara la Asia ambao raia wake wanasafiri katika makundi makubwa itaongeza idadi na mapato na kufikia adhma ya serikali kabla 2025."

Hifadhi hiyo yenye ukubwa wa kilomita za mraba 3,234, ni miongoni mwa Hifadhi za Taifa 22 zilizopo nchini kwa sasa, ikiwa chini ya miteremko ya safu ya Milima ya Tao la Mashariki. Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi, ilianzishwa kama Pori la Akiba, lililomegwa kutoka Pori la Akiba la Ruvu Mwaka 1951.

Ofisa Mhifadhi Mkuu, Kitengo cha Utalii wa Mkomazi, Happiness Kiemi, alimwahidi Naibu Waziri huyo, kwamba watalifanyia kazi agizo hilo, pamoja na suala la utatuzi wa migogoro ya wanyamapori waharibifu.

Alisema hifadhi hiyo imeboresha miundombinu ya utalii, ikiwamo ujenzi wa lango la kuingilia wageni pamoja na viwanja vya ndege ili kurahisisha safari za kuingia hifadhini na kutoka.

Katika kuboresha shughuli za utalii katika hifadhi hiyo, pamoja na mambo mengine, TANAPA iko mbioni kufungua malango matano katika eneo la Kisiwani na Njiro, Wilaya ya Same, Komakota Wilaya ya Lushoto, Umba-Mkinga na Ndea iliyoko Wilaya ya Mwanga.

**"Hakuna haja ya kuachia makundi makubwa ya watalii wanaozuru Zanzibar kuondoka, wakati mmeboresha viwanja vya ndege. Ni wajibu wa TANAPA kutumia fursa na mikakati ya kuwashawishi watalii kutoka Zanzibar kuja kuwaona Faru na wale wanyama wakubwa watano.**

# TAMISEMI kuwanyang'anya leseni watumishi afya kifo cha mjamzito

**Na Oscar Assenga,** MUHEZA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema baada ya ripoti ya uchunguzi wa tuhuma za kifo cha mjamzito, Mariam Zahoro (39) na kichanga chake kukamilika, itachukua uamuzi mgumu, ikiwamo kunyang'anya leseni za watumishi wa afya watakaobainika.

Mariam na kichanga chake, walipoteza maisha Novemba 11, mwaka huu, katika Kituo cha Afya cha Kabuku kilichoko Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga, kwa madai ya kukosekana Sh. 150,000 gharama ya kufanyiwa upasuaji.

Naibu Katibu Mkuu (TAMISEMI), anayeshughulikia afya, Dk. Wilson Mahera, alisema serikali itawapoka leseni hizo wale watakaobainika walifanya uzembe katika kituo hicho.

Aliyasema hayo jana, akiwa Wilaya ya Muheza, ambako alikwenda kukagua maendeleo ya utoaji huduma katika Hospitali ya Wilaya hiyo.

Dk. Mahera, alisema serikali imefanya uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya afya ili wananchi wapate huduma bora, hivyo wao kama wasaidizi wa Rais, Samia Suluhu Hassan, hawatakubali kuona watumishi wanakiuka maadili.

Novemba 14 mwaka huu, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alitoa maelekezo kwa Baraza la Madaktari Tanganyika (MCT) na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania (TNMC), kuhakikisha ndani ya siku saba wanampelekea taarifa ya kifo cha mjamzito na kichanga chake kilichotokea Novemba 11 mwaka huu, ambako jana ni siku ya mwisho.

Waziri Ummy aliwahakikishia Watanzania kuwa, baada ya kupokea taarifa ya uchunguzi, kila mtumishi aliyehusika atachukuliwa hatua kali za kitaaluma, kiutumishi na kijinai, ikiwamo kufikishwa mahakamani mujibu tuhuma za kijinai pale itakapothibitika.

Wanaochunguzwa kwa mujibu wa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, Omari Mkangama, ni watumishi watatu walioshiriki kumpa-



Waziri wa Madini, Anthony Mavunde (kushoto), akimsikiliza Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (katikati), baada ya kutembelea mgodi wa Tanzanite ulioko kitalu C unaomilikiwa na Franone Mining LTD katika Mji Mdogo wa Mirerani hivi karibuni. Wa pili kushoto ni Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Onesmo Mbise. **PICHA: GIFT THADEY**

# Teknolojia ya kilimo ikolojia yaanza kutumika rasmi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

VIKUNDI 20 vya wakulima na wafugaji katika Mkoa wa Kilimanjaro, vimeanza rasmi kugeukia 'kilimo ikolojia' kinachopunguza matumizi makubwa ya upuliziaji wa kemikali za sumu kwenye mimea inayotumika kwa uzalishaji wa chakula.

Akizungumza jana, wakati wa mafunzo kuhusu mfumo huo, Mratibu wa Mtandao wa Vikundi vya Wakulima na Wafugaji, Mkoa wa Kilimanjaro (MVIWAKI), Alex Urio, alisema wao kama wadau wakuu wa kilimo ikolojia, wamejikita zaidi kuwajengea uwezo wakulima na wafugaji kuhusu urejeshaji wa baionuai, mbinu za utunzaji wa mazingira na matumizi ya mbegu za asili.

Alisema kilimo ikolojia, kina mfumo jumuishi wa uzalishaji unaotegemeana, ambao unapunguza uharibifu, huku ukiwa na mwingiliano wa kirafiki wa viumbe hai vilivyoko ardhini.

Urio alisema wakulima wengi nchini, hawana uwezo wa kumudu gharama za kununua dawa na mbolea, kwa ajili ya kustawisha mashamba na kuua wadudu na magonjwa kwenye mazao yao. Kwa hiyo kilimo ikolojia, kinaweza kuwa msaada mkubwa kwa wakulima na jamii za kifugaji.

"Kilimo ikolojia ni mbinu shirikishi iliyounganishwa, ambayo inatumika kwa wakati mmoja kwa kutumia dhana, kanuni za ikolojia na usimamizi wa mifumo endelevu ya kilimo na chakula," alisema.

Alisema mfumo huo unalenga kuboresha mwingiliano kati ya mimea, wanyama, binadamu na mazingira. Pia kinashughulikia hitaji la mifumo ya chakula yenye usawa wa kijamii, ambayo watu wanaweza kufanya uchaguzi juu ya kile wanachokula, jinsi na wapi kinazalishwa.

Mmoja wa wataalamu wa kilimo, Mosses Anney, alisema licha ya umuhimu wa kilimo hicho, kinapewa umuhimu kidogo katika sera za Tanzania, huku kikisuasua kwa mchakato wa kufanya uamuzi na uthubutu mdogo wa waandaaji programu wa maendeleo vijijini.

Kwa mujibu wa Anney, tatizo jingine ni uelewa mdogo wa kukuza wakulima wadogo, kupata fursa za kilimo endelevu kupitia kilimo ikolojia.

Kwa mujibu wa Wizara ya Kilimo, kilimo mwaka jana kilichangia asilimia 24.1 ya pato la taifa (GDP), asilimia 30 ya mapato ya usafirishaji wake nje ya nchi, na kinaajiri Watanzania kwa asilimia 73. Wastani wa ukuaji wa kilimo, ni asilimia 4.4 ambayo haitoshi kuleta utajiri mkubwa na kuondoa umaskini.





# Kikosi kazi chaundwa kupambana na utoroshaji wa madini Kahama

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MGODI wa Kembo Gold Mine and Partners uliopo Kata ya Zongomela Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, umeanzisha kikosi kazi cha kupambana na watoroshaji wa mawe yanayosadikiwa kuwa na madini ya dhahabu mgodini pamoja na kudhibiti utumikishwaji watoto mgodini hapo.

Katibu wa Mgodi huo, Cosmas Magati, aliyabainisha hayo juzi wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari vilivyofika mgodini hapo kuangalia namna walivyochukua hatua ya kukabiliana na mvua za El-nino.

Alisema, mgodi huo kwa sasa unatumia geti moja kuingilia na kutokea na wamefanya hivyo kwa lengo la kukabiliana na wachimbaji wasiokuwa waadilifu ambao wamekuwa wakitorosha mawe yanayosadikiwa kuwa na dhahabu na kusababisha serikali kukosa mapato.

Vilevile alisema wameanzisha kikosi kazi kwa ajili ya kupambana na watu hao pamoja na kudhibiti uwepo wa ajira za watoto wenye umri chini ya miaka 18 katika maeneo ya machimbo kwa kuwachukulia hatua wale wote wanaonekana kuwatumikisha.

Alisema watoto wamekuwa wakitumika mgodini hapo katika uchotaji wa maji, mchanga wenye madini pamoja na mawe hivyo watakaobainika kufuatia msako wa kikosi hicho watachukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kuondolewa eneo hilo.

Meneja wa Mgodi huo, Solomon Mataba, alisema wamejenga mtaro mkubwa kuzunguka eneo la mgodi ili maji ya mvua yasipenye ndani ya mgodi hali itakayosaidia maduara ya wachimbaji wadogo kutokujaa maji na kuleta maafa.

Alisema, wanajenga vyoo kwa kisasa ili kulinda mazingira yasichafuliwe na wachimbaji na wanunuzi kwa kujisaidia ovyo vichakani na kusababisha kuibuka kwa magonjwa ya mlipuka hasa kipindupindu.

Mkurugenzi wa Mgodi huo, Erenest Maganga, alisema wanawake wachimbaji wamewapatia kipaumbele katika kupata maeneo mazuri ya kuchimba na baadhi yao wanachimba na wengine wameingia ubia na vijana, wananunua mawe yanayosadikiwa kuwa na madini na kwenda kusaga na kujiingizia kipato.

Alisema, awali walikuwa na dhana potofu kuwa mwanamke akionekana maeneo ya uchimbaji, madini yanakimbia jambo ambalo lilikuwa sio kweli kwani katika Mgodi mdogo wa Nyamishiga uliopo Lunguya-Msalala wachimbaji hao wanafanya vema na maduhuri ya serikali wanalipa kulinganisha na wachimbaji wanaume..



Mchimbaji mdogo katika Mgodi wa Kembo Gold Mine and Partnes, Salome Shilinde, ulioko Kata ya Zongomela, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, wilayani Kahama mkoani Shinyanga, akiosha mchanga unaosadikiwa kuwa na madini ya dhahabu kwa kutumia njia ya kienyeji jana. **PICHA: SHABAN NJIA.**

# UVCCM Shy yatimba vyuoni kusaka wanachama

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

VIONGOZI wa seneti ya vyuo na vyuo vikuu Mkoa wa Shinyanga wa Umoja wa Vijana CCM (UVCCM), wameanza kuzunguka katika vyuo vyote mkoani humo kwa lengo la kutafuta na kusajili wanachama wapya na kutoa elimu ya itikadi ikiwa ni sehemu ya kukiimarisha chama hicho.

Mwenyekiti wa seneti mkoani hapa, Said Sultan, akizungumza juzi katika Chuo cha Afya za Sayansi Kolandoto, alisema hatua hiyo ni endelevu kwa kupita katika vyuo vyote mkoani humo, pamoja na kufungua matawi mapya ya seneti ili kukiimarisha Chama kuelekea uchaguzi ujao.

Alisema viongozi bora wanaanza kupikwa wakiwa shuleni na kwenye vyuo kwa kupewa mafunzo ya Itikadi ili wawe wazalendo na nchi yao na kushiriki kikamilifu katika shughuli za kitaifa ukiwamo uchaguzi.

"Mtaji wa chama chochote ni kuwa na wanachama wengi na hii inakuwa msaada katika kushinda uchaguzi wa aina yoyote hivyo kuzunguka kwetu katika vyuo ni kuongeza idadi ya wapiga kura wa CCM," alisema Sultan.

Katika hatua nyingine Sultan, alipongeza serikali kupitia bodi ya mikopo kwa wanafunzi kwa kuanza utoaji wa mikopo katika vyuo vya kati, hali ambayo imesaidia wanafunzi wanaotoka zenye uwezo mdogo kifedha kupata fursa ya kusoma na kutimiza ndoto zao.

Naye Mwenyekiti Mstaafu wa Seneti kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Pius Mwandu, akitoa elimu ya darasa la Itikadi, aliwataka wanafunzi hao kuwa Wazalendo na nchi yao, kupendana kama ndugu ikiwa ni pamoja na kuisaidia serikali katika utekelezaji wa majukumu yake bila kujali nyadhifa zao.

Mkuu wa Chuo cha Sayansi za Afya Kolandoto, Paschal Shiluka ambaye alichaguliwa kuwa Mlezi wa Senet katika chuo hicho, aliwasihi vijana hao kuhakikisha wanafuata sheria na taratibu za nchi katika utekelezaji wa majukumu yao ya chama kwa kuzingatia vilevile kuweka bidii katika masomo.

# Waandishi wa habari wahimizwa kuleta mabadiliko katika tasnia

**Na Timothy Itembe,** MARA

MKURUGENZI Mtendaji wa Muungano wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), Kenneth Simbaya, amekutana na kufanya mazungumzo na waandishi wa habari mkoani Mara akiwahimiza kuwa na dira katika shughuli zao za uandishi na klabu yao ili kuleta mabadiliko katika tasnia ya habari.

Simbaya alitoa kauli hiyo juzi katika semina ya siku moja na waandishi hao wa habari mkoani hapa na kuwataka kuwa na dira itakayowasaidi kujiimarisha katika utendaji kazi na kupiga hatua kimaendeleo.

Alisema umoja huo hautokuwa tayari kusimama na klabu nyingi haziendani na mfumo wa kiutendaji bali watasonga mbele na klabu ya waandishi ambayo imekubali na kuridhia kusonga mbele kwa vitendo kwa kufuata dira yao. "Mabadiliko ni lazima wala sio ombi, mabadiliko yoyote ya taasisi yanatokana na mtu mmoja mmoja hiyo kama waandishi hakikisheni hamfanyi kazi kwa mazoea bali jiwekeeni malengo katika utendaji kazi wenu na kusaidia klabu kuwa na ufanisi," alisema Simbaya.

Makamu Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Mara (MRPC), Raphael Okelo, alisema ili kufikia mabadiliko katika dira na mfumo mmoja ni lazima waandishi wa habari wawe na lugha moja itakayoleta mafanikio ya kiutendaji.

"Pia ipo haja ya kuimarisha mifumo ya ushirikiano ikifuatiwa na kufanya kazi kwa weledi ili jamii inayotuzinguka kutuamini na kutushirikisha katika shughuli mbalimbali pindi zinapojitokeza," alisema.

Katibu wa MRPC, Pendo Mwakembe, alisema taasisi na wadau wa habari kwa ujumla wanatakiwa kujali vyombo vya habari na kuwatumia waandishi wa habari kwa maendeleo ya Taifa na si vinginevyo.

Aliwashauri waandishi hao kubuni miradi ya klabu ya kuwaingizia kipato kuliko kuendelea kuwa tegemezi kwa wadau na taasisi mbalimbali hali inayowaweka katika hatari ya kujiingiza katika mitego ya rushwa.

Baadhi ya waandishi wa habari washiriki waliohudhuria semina hiyo akiwamo Helena Magabe aliomba UTPC kubadili mfumo wa upatikanaji wa washiriki katika semina na shughuli mbalimbali za waandishi kwani imeonekana watu wanajirudia hali inayowakosesha fursa waandishi wengine wenye uhitaji wa kuongeza uelewa.





Ukurasa 12

WFT-T, wadau wanavyopambania kuwanusuru wafanyakazi wa ndani



Ukurasa 14

**Faraja kinamama wagumba wanapoambiwa kuzaa kwaja**

Nipashe
# TESA
Jumanne Novemba 21, 2023
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

ELIMU
NA SABATO KASIKA

SIKU 16 KUPINGA UKATILI KIJINSIA

VITUKO UNYANYASAJI

# Hata leo wanaume huwakataa, kuwakimbia pacha, eti mkosi

- Mwanamama Diana aguswa, atamani watambulike rasmi



Mwenyekiti wa Eden Twins Foundation, Diana Mbena, akitoa msaada kwa Amina Abdallah aliyejifungua pacha Novemba 11, mwaka huu katika Hospitali ya Rufani ya Ilala jijini Dar es Salaam. **PICHA: SABATO KASIKA**

WIKI hii ni mwanzo wa Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia Duniani zikiaanza Novemba 25 na kufikia tamati Desemba 10.

Kama kawaida lengo ni kuhamasisha mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na wasichana pamoja na watoto ili kuwa na jamii yenye kuthamini watu wote na kuwapa fursa sawa.

Wakati kampeni hiyo ikielekea kuzinduliwa, Mwenyekiti wa Taasisi ya Eden Twins Foundation (ETF), iliyoko mkoa wa Pwani, Diana Mbena, anasema ukatili ni tishio ukiumiza hata watoto pacha na mama zao.

Anaeleza kuwa wapo wanawake wanaozaa pacha na kutelekezwa, mambo anayoyafichua katika mazungumzo na gazeti hili jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

Anasema amebaini kuwa baadhi ya wazazi wa pacha hawana uwezo kimapato, hivyo kukosa chakula, mavazi, tiba na kushindwa kuwatunza watoto.

"Mbaya zaidi, wengine wanatelekezwa na waume kwa sababu nyepesi, wapo wanaodai kuwa kuzaa pacha ni mkosi au balaa na kuhoji inakuwaje, wakati katika familia zao hazina pacha?" Anasema Diana.

Mwanamama huyu ameyabaini hayo alipoanzisha taasisi hiyo mwaka 2021, baada ya kuhudumia familia yenye pacha watatu Kibaha mkoani Pwani ambayo ilikuwa na maisha duni.

Mwenyekiti Diana anafafanua kuwa baada ya kuanzisha shirika hilo, aliitambulisha kwenye vyombo vya habari ili kuwavuta wenye changamoto hizo kujitokeza wakiwamo wenye watoto hao wanaoishi maisha duni.

Anawataja kuwa walitoka mikoa ya Pwani na Dar es Salaam na kwamba kati ya 29 waliojitokeza, 25 kati yao wamekimbiwa na waume zao, huku wanne ndio wanaendelea na ndoa zao.

"Kwa hiyo ukiangalia idadi hiyo utagundua kuwa kuna tatizo ambalo linahitaji msaada zaidi kutoka serikali na wadau, ili kundi hili litambuliwe rasmi na kusaidiwa," anasema.

Anamtaja mmoja wa waliotelekezwa mkazi wa Makoka Dar es Salaam (jina tunalo), anayelea watoto wake watatu baada ya kutelekezwa na mumewe, aliyedai hana uwezo wa kuwalea.

Mama huyu anakiri kutelekezwa akiwa nyumbani kwao Singida na mimba ya miezi nane na kuamua kukimbilia Dar es Salaam kutafuta msaada hatimaye akaisikia taasisi hiyo na kuifuatilia.

"Nimejifungulia Dar es Salaam, nikahangaika na pacha wangu watatu, hadi nilipowapata Eden Twins Foundation wakanipa msaada wa hali na mali na sasa ninaweza kumudu maisha yangu na kulea wanangu na wana mwaka mmoja na nusu sasa," anasema.

Anasema kwa sasa ni mama lishe japo awali alikuwa amekata tamaa ya maisha huku akifuatwa na baadhi ya wamiliki wa vituo vya kuleta watoto wakitaka wachukue watoto wakawalee, lakini alikataa kuwaachia.

Aidha, Diana akizungumzia ukubwa wa tatizo, anasema iwapo utafanyika utafiti kwa nchi nzima inawezekana kukawa na wanawake wengi waliozaa mapacha na kutelekezwa na waume zao.

"Vitendo vya baadhi ya wanaume kukimbia familia kwa sababu ya kuzaa pacha ni ukatili wa kijinsia, hivyo wakati huu wa kuelekea Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, sauti zingepazwa kuokoa kundi hili," anasema.

Kadhalika, anasema anatamani Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Makundi Maalum, kuwatambua na kuwapigania kama inavyopigania na makundi mengine ya wanawake, wasichana na watoto.

INAENDELEA UK.14

ELIMU
NA MWANDISHI
WETU

# WFT-T, wadau wanavyopambania kuwanusuru wafanyakazi wa ndani

• Ni juhudi ili wajiamini, kujua mishahara, sheria na kuandika mikataba ya ajira

WATU wengi kwanini wanatesa wafanyakazi wa ndani? Inawezekana nawe ni mmoja wao. Wakati unasaka jawabu fahamu kwamba ukatili dhidi yao ni matendo yanayohusisha unyanyasaji wa kimwili, kingono, kihisia na kiuchumi.

Ukiangalia unyanyasaji kiuchumi unaumiza, ikihusisha kunyimwa mkataba wa ajira, kutolipwa, kupunjwa na hata kukatwa mshahara pale mfanyakazi anapodaiwa kusababisha hasara kama kuvunja vyombo au kuunguza vyakula ni mifano yapo mengi.

Kuwatesa kimwili ni pamoja na kuwapiga, kuwajeruhi, kunyimwa chakula wakati kwenye hisia wanatukanwa, kuudhiwa na kebehi nyingi kama kuitwa mchafu, usiyeshiba, 'mkijiji' na wengine kudaiwa wachawi.

Ikumbukwe kushindwa kuchukua hatua kuwasaidia wafanyakazi wa nyumbani, kunasababisha madhara kwa kundi hili, ndiyo maana Mtandao wa Wafanyakazi wa Nyumbani Tanzania umeundwa, ili kutetea kuwapo na ajira au kazi zenye staha, zinazoheshimu utu wa mtu, haki zake kwa mujibu wa sheria na heshima kwa anayefanyakazi hizo.

Mtandao ukitetea kuwa lazima kuwe na ajira za nyumbani zenye staha unasisitiza usalama wa watumishi hao kwa mfano wakati wa UVIKO -19 ulifanyakazi ya ziada kuwatetea wanachama wake ili walindwe kuepushwa na maradhi ya COVID-19 yaliyoingia nchini 2020.

"Wakati huo tuliwahamasisha na kukumbusha waajiri kuwalinda wasiambukizwe corona. Mathalani kutumwa maeneo yenye watu wengi kama sokoni, hospitalini au kwenye vituo vya mabasi bila barakoa, vitakasa mikono na glovu pale inapobidi. Tulifanya hivyo ili kuwaepusha na maradhi," anasema Demitila Faustine.

Demitila Mratibu wa Miradi wa Mfuko wa Ruzuku kwa Mashirika ya Wanawake (WFT-T), anasema hayo anapozungumza na Nipashe kuhusu majukumu na jinsi mfuko unavyosaidiwa na wanawake kwenye sekta ya ajira za nyumbani.

Anaongeza kuwa mbali na ulinzi dhidi ya UVIKO -19, wanachama wa mtandao wamewajengewa uwezo wafanyakazi hao ili kujiimarisha na kujikinga na unyanyasaji na ukatili wa kijinsia.




Demitila Faustine, Mratibu wa Miradi wa Mfuko wa WFT-T, akielezea mafanikio kwa wadau wakati wa Tamasha la Jinsia 2023.
**PICHA ZOTE: MWANDISHI WETU**

> Wasichana wameruhusiwa kujiunga na vikundi au mtandao wa watumishi wa ndani. Wapo wengine wamejiari wana saluni zao, wanasuka, wanajitokeza kuzungumzia matatizo yao.

Anaongeza kuwa ni hatua zinazochukuliwa kwa pande zote, waajiriwa, waajiri wao, viongozi wa serikali za mitaa na idara ya ustawi wa jamii.

Demitila, anafafanua kuwa mfuko wa WFTT unafanyakazi na Mtandao wa Wafanyakazi wa Nyumbani Tanzania kuwajengea uwezo kufunguka na kutoa taarifa kwa viongozi wakifanyiwa ukatili.

"Tunawafundisha na kuwaonyesha mifano ya mikataba ya ajira ya maandishi ili wasifanye kazi bila mkataba, wanafundishwa sheria ya ajira na mahusiano kazini na tamko la serikali kuhusu kiwango cha mshahara cha watumishi wa ndani." Anasema Mratibu wa Miradi wa WFT-T.

Kwa mujibu wa tangazo la serikali No: 687/2022, viwango vya mishahara yao ni pamoja na Shilingi 60,000 anayeishi na mwajiri Shilingi 120,000 anayefanyakazi lakini hakai nyumbani kwa mwajiri Shilingi 210, 000 kwa walioajiriwa na maofisa wenye stahiki na wafanyabiashara wakubwa wakati 250,000 ni mshahara wa anayefanyakazi kwa wanadiplomasia.

Anafafanua kuwa eneo la watumishi wa ndani linahusisha wanawake zaidi wakiwamo hata mabinti chini ya miaka 19 na kazi ya kutafuta ustawi wao lazima ihusishe waajiri wao, jukumu analosema limefanyika kwa kushirikiana na maofisa maendeleo ya jamii na wenyeviti wa serikali za mitaa na hata maofisa elimu kata kwenye mikoa wanayotoa elimu na kuhamasisha mabadiliko.

Akitoa mifano ya kazi zilizofanyika Mwanza wilaya za Ilemela na Nyamagana, anasema pamoja kuwafahamishwa kuhusu kazi za staha, mikataba ya maandiko, mishahara kwa mujibu wa sheria, wanahimizwa pia umuhimu wa kupima afya za wafanyakazi hao.

"Mtandao huu unaoundwa na mashirika tofauti ya wafanyakazi wa nyumbani wanaotetea haki za wanawake na wasichana wanaofanyakazi za ndani , tuna mengi ya kujivunia, mfano kukubalika na jamii na kazi zzetu kuwa na mafanikio. Tumaona kuna mwitikio mkubwa kwenye jamii na baadhi zimeacha tabia hasi za kuwanyanyasa watumishi wa ndani.

"Wasichana wameruhusiwa kujiunga na vikundi au mtandao wa watumishi wa ndani. Wapo wengine wamejiari wana saluni zao, wanasuka, wanajitokeza kuzungumzia matatizo yao.

Wengine hufikisha malalamiko serikalini. Kiuchumi wapo waliofungua akaunti wanaweka akiba na pia mishahara hupitia benki badala ya kuwapa jamaa zao,wazazi au walezi," anaongeza Demitila.

Wapo wanaojiongeza zaidi baada ya kujua sheria wameboresha mahusiano na waajiri wanapotaka kuondoka wanatoa taarifa na kuwaacha waajiri wakiwa wamejiandaa bila usumbufu hata kusaidia kupata watumishi wengine.

### KUWA NA HIFADHI

Demitila anasema suala la wasichana au watumishi wa ndani kutoroka limeumiza wengi na WFTT imesaidia kulitatua, mfano mkoani Mwanza wana kituo cha kuwatunza walionyayanyaswa kama kufanyiwa ukatili wa kingono, kupigwa au kufukuzwa bila msaada.

Anaongeza kuwa pamoja na kutoa hifadhi, kinawasaidia kumfuatilia mwajiri aliyefanya uhalifu ili alipe stahiki au kupelekwa kwenye vyombo vya haki ili mfanyakazi asidhulumiwe, lakini nyumba hiyo ya hifadhi inawanusuru watoto waliotumikishwa kazi za ndani na kuachishwa masomo.

Wanarejeshwa shuleni hasa wenye chini ya miaka 18 au kuwaunganishwa na familia zao, aidha nyumba inawatunza na kuwaunganisha na taasisi za kuwahudumia au kuwarejesha kwa familia zao wahanga wa biashara haramu ya kusafirisha binadamu hasa wanawake na watoto, anafafanua Demitila.

"Hadi 2021, nyumba yetu inayoitwa WoteSawa Shelter Mwanza ilikuwa imeokoa waathirikia 92 wakiwamo wa unyanyasaji kingono, kiuchumi hasa waliopunjwa au kunywa mishahara, ajira za utoto na waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu," anaongeza.

Japo, anasema mtandao wa wafanyakazi wa ndani una mafanikio lakini changamoto kubwa ni uhitaji mkubwa wa kuwafikia na kuwahudumia wasichana maelfu walio kwenye majiji, miji mikubwa na midogo.

Hadi mwaka jana watumishi wa ndani zaidi ya 1,400 walikuwa wamefikiwa na kuelimishwa kuhusu haki na stahiki zao, sheria za kazi, ujira, afya zao na kuripoti matendo ya unyanyasaji kuanzia wa kingono na ukatili wowote wanaokutanao nao.

Beatrice Johnson ni Mkurugenzi Mtendaji Asasi ya Light for Domestic Workers(LDW), iliyoko Morogoro pia ni Katibu Mtendaji wa Mtandao wa Wafanyakazi wa Nyumbani Dodoma na katika kushirikiana na wana mtandao wamewafika wafanyakazi za ndani katika kata kadhaa za wilaya ya Morogoro Mjini na mbili za Dodoma.



Mkurugenzi Mtendaji LDW, Beatrice Johnson, kushoto, akizungumzia mafao ya kazi zenye staha kwa watumishi wa nyumbani.

Anaiambia Nipashe jijini Dar es Salaam hivi karibuni kuwa ni mfanyakazi wa ndani na aliingia katika jukumu hilo ili kukwepa ndoa za utotoni nyumbani kwao Dodoma kwa sababu alilazimishwa kuozwa udogoni na akajinusuru kwa kuomba kazi kama mtumishi wa ndani.

"Baada ya kujitambua mwaka 2018 nilianzisha asasi ya kijamii CBO iliyowaunganisha pamoja watumishi wa ndani ili kuifunza jamii tunayoifanyia kazi kubadilikia na kuachana na mitizamo hasi dhidi ya wafanyakazi wa ndani. Ninafanya hayo nikiwa Morogoro mjini.

"Tulijiunga pamoja wasichana 15 tukaanza kuchanga kila mwezi Shilingi 5,000 tukaanzisha mfuko na kuanzisha harakati za kuwatembelea wenzetu na kuwahamasisha kuhusu haki zetu, ukatili kijinsia na kuhimiza kujiamini ili kuleta mabadiliko."

Mwaka 2021 WFT-T iliwaunga mkono na kufadhili kazi zao ikiwawezesha kubadilisha asasi yao CBO kuwa shirika (NGO) na kuendeleza juhudi za kubadilisha mitizamo hasi dhidi yao, kuelimisha waajiri, watumishi wa ndani.

Hadi mwaka jana waajiri 172 pamoja na viongozi wa serikali za mitaa madawati ya jinsia, ya polisi na ya ustawi wa jamii waliwafikia kuwapa mafunzo ya haki, sheria za kazi na mikataba ya ajira kwa watumishi wa nyumbani, anasema.

"Tatizo la kukosa uelewa wa sheria lilisababisha serikali za mitaa kushidwa kutatua migogoro ya wafanyakazi wa ndani. Tuliwapa mafunzo na sheria zinazohusika na hatua za kuwasaidia. Tuliwahamasisha viongozi wa kata 15 za Manispaa ya Morogoro. Kwa pamoja zaidi ya watu 250 tumewafikia kuanzia wasichana zaidi ya 150, waliopata mafunzo viongozi wa serikali za mitaa na ustawi wa jamiii," anasema.

### UKOMBOZI KIUCHUMI

Victoria Paschal ni 'zao' la LDW Morogoro anayesema hamasa na kazi zinazofanywa na Mtandao wa Wafanyakazi wa Nyumbani, maisha yamebadilika.

Baada ya kuajiriwa kwa miaka 10 akiwa mkoani Morogoro anasema elimu, hamasha pamoja mafunzo ya ujasiriamali aliyopata amejifunza kushona nguo na sasa ni fundi mahiri akishiriki na wana mtandao kuwapa mafunzo ya ujasiriamali wafanyakazi wa ndani.

Anasema mtandao huo umefundisha ujuzi na ujasiriamali na kwamba Mwanza kuna kituo cha kujifunza ushonaji na wasichana takribani 521 mwaka 2021 walikuwa wamenufaika na wanawasiliana.

Mtandao wa kuwasaidia wasichana wanaofanyakazi nyumbani umesambaa sehemu nyingi nchini na NIpashe inakutana na Farida Daniel, kutoka Initiative for Domestic Workers Bagamoyo, inayojishughilisha na ustawi wao, mkoani Pwani.

> Tatizo la kukosa uelewa wa sheria lilisababisha serikali za mitaa kushidwa kutatua migogoro ya wafanyakazi wa ndani. Tuliwapa mafunzo na sheria zinazohusika na hatua za kuwasaidia.

Farida anasema kwa kushirikiana na mashirika ya mtandao, huo wanafanyakazi katika kata ya Magomeni ambako wameunda vikundi tisa vyenye wanachama takribani 150 ambavyo vinanufaika na mafunzo, elimu ya ujasiriamali, haki na stahiki zao na masuala ya kubadilika kiuchumi.

"Pamoja na kutetea ustawi wa watumishi wa ndani , tunashirikiana na wadau kukomesha ajira za watoto na usafirishaji haramu wa binadamu. Tunafanyakazi na mtandao na tumebaini kuna watoto husafirishwa kwa ahadi hewa na udanganyifu kuwa wanapelekwa mjini kwenye mashirika kusomeshwa au kuendelezwa lakini sivyo wanadanganywa ili wapelekwe kwenye madanguro au kwenye kuuza baa yote yakiathiri ustawi wao," anasema Farida.

Mtandao unawaunganisha na mashirika ya kupinga usafirishaji haramu wa binadamu ili kuwarudisha shuleni watoto na kuwaondoa kwenye ajira haramu na pia kuchukua hatua, anasema.

Kwenye kuwatetea wafanyakazi wa nyumbani wanawafundisha sheria za kazi, viwango vya mishahara na kipinga ukatili kijinsia, kuingia mikataba ya maandishi baina yao, waajiri na viongozi wa serikali na mitaa na wasikubali mkataba usio na pande hizo tatu.

ELIMU
NA MWANDISHI WETU

# Faraja kinamama wagumba wanapoambiwa kuzaa kwaja

## • Waziri Dorothy Gwajima aahidi serikali itawabeba

UGUMBA japo unazihusu pande zote mwanamke au mwanamume, 'balaa' ni la mwanamke ambaye shida humwelemea zaidi akinyanyaswa, kufukuzwa au kutelekezwa pale ndoa inapovunjwa kwa lawama kuwa amekosa mtoto.

Mara nyingi furaha ya ndoa hasa kwa Waafrika ni kuwa na watoto na wanapokosekana lawama ni kwa mama ambaye analaumiwa kwa maneno na kejeli za kutoka familia na ndugu wa mume kuwa hazai.

Kwa mujibu wataalamu wa afya, wanandoa wakiishi pamoja kama mke na mume kwa zaidi ya mwaka mmoja au zaidi ya miezi 12 na kushiriki tendo la ndoa mara kwa mara na ikatokea hawapati mtoto ni moja ya dalili ya ugumba.

Shirika la Afya Dunia (WHO) hivi karibuni limeripoti kwamba, mwanandoa mmoja kati ya sita duniani ana tatizo la ugumba na kwa mujibu wa tovuti ya Wizara ya Afya, ugumba ni tatizo kubwa nchini lakini mpaka sasa hakuna takwimu rasmi za kitaifa.

Ili ulifanyika utafiti mdogo ambao unaonesha asilimia 30 ya watu wana tatizo hilo, inakadiriwa kuwa katika kila mahusiano ya wenza wanne, mmoja kati yao anakua na tatizo la kupata watoto, ambazo ni takwimu za kidunia.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Kinamama na Uzazi, wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga Dk.Augustino Maufi, anasema katika kliniki ya magonjwa hayo inayofanyika mara mbili kwa wiki asilimia 30 hadi 40 shida yao kubwa ni tatizo hilo.

Anasema wanawake hao ambao hukutwa na tatizo la ugumba hali hiyo huchangiwa na kuziba mirija ya uzazi na kuongeza: "Tatizo la ugumba kwa wanawake katika mkoa wa Shinyanga ni kubwa, ukiangalia kwenye kliniki yetu inayofanyika mara mbili kwa wiki, Jumatatu na Alhamisi shida hiyo ipo," anasema Dk. Maufi.



Waziri Dorothy Gwajima (kushoto), Mtendaji MKuu wa Merck Foundation, Dk. Rasha Kelej. **PICHA: MTANDAO**

Anataja baadhi ya sababu kubwa ambazo zimekuwa zikisababisha wanawake kukabiliwa na matatizo ya ugumba, kuwa ni utoaji mimba ovyo, matumizi holela ya dawa ya kuzuia mimba ikiwamo P2, maradhi katika mfumo wa uzazi, magonjwa ya ngono kikiwamo kisonono na kusababisha mirija ya uzazi kuziba.

Anafafanua kuwa baadhi ya kinamama wakianza tiba ya tatizo la ugumba ikiwamo kuzibua mirija ya uzazi, hukutana na washauri wengine mitaani na kusitisha dozi na kuanza kutumia njia nyingine ikiwamo kwenda kwa waganga wa kienyeji, na wanapokwama hurudi hospitali huku tatizo lake likiwa sugu na kusababisha uwezekano wa kupata mtoto kuwa mdogo zaidi.

Aidha, anasema tatizo la ugumba halipo kwa wanawake hata wanaume nao wanakabiliwa nalo kwa sababu mbegu zao kushindwa kutunga mimba au kurutubisha yai na kutoa wito kwa wanandoa ambao wanakabiliwa na tatizo la kukosa watoto ndani ya mwaka mmoja, wahudhurie wote kwenye huduma za afya ili wachunguzwe na kutibiwa.

Mwanandoa mmoja, jina tunalo anasema baada ya kuwa kwenye ndoa na kushindwa kushika mimba kwa miwili, ilibidi ivunjike kutokana na upande wa mume wake kumshambulia kuwa hana faida kwao sababu hazai. Baada ya kashfa na matukano mengi aliachwa na sasa anaendelea na maisha yake.

### WANAUME WAPO

Mwingine anayezungumzia ugumba ulivyomwathiri jina tunalo pia, anasema alifunga ndoa mwaka 2017 na baada ya kumaliza mwaka mmoja bila ya kupata mtoto ndugu za mumewe walianza kumshambulia wakitaka waachane na akapata manyanyaso mengi yaliyomuumiza kisaikolojia, kiafya na hata kimwili.

Anasema baada ya manyanyaso hayo kuendelea, ilibidi waende hospitali kupimwa na vipimo vikaonyesha kuwa tatizo si lake bali ni mumewe kuwa mbegu zake hazina uwezo wa kurutubisha mayai na hivyo kushindwa kumpa mkewe mimba na kuhitaji matibabu.

### GHARAMA KUPUNGUA

Tovuti ya Wizara ya Afya, inazungumzia suala la kupandikiza mimba ikisema kuwa serikali itarejea upya gharama za upandikizaji wa mimba kwa watu wenye matatizo ya uzazi hasa kukosa watoto, ili kuwapunguzia mzigo wa gharama kubwa endapo watajiunga na bima ya afya kwa wote, ni maelezo yanayomnukuu Waziri Ummy Mwalimu.

Gharama za upandikizaji mimba katika baadhi ya hospitali jijini Dar es Salaam, huduma hugharimu kuanzia Shilingi milioni 13 hadi 17 kutegemea na aina ya huduma inayohitajika.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima, hivi karibuni akizungumza na Nipashe akiwa India kwenye Mkutano wa Taasisi ya Merck Foundation, anasema wanawake wenye matatizo ya ugumba hawapaswi kunyanyapaliwa bali kupendwa na kusaidiwa ili kutibiwa na kupata watoto.

Anasema Tanzania kwa kushirikiana na taasisi hiyo ya kimataifa Merck Foundation, wamekuwa wakitafuta namna ya kusaidia wanawake wenye matatizo ya ugumba ili wapate watoto na hata kufikia hatua ya kusomesha madaktari 42 ambapo 15 wamesomea ujuzi wa kusaidia wanawake wenye ugumba kwa matibabu na kupata watoto.

"Si vyema kunyanyasa au kuwanyanyapaa wanawake ambao wana matatizo ya ugumba hasa wale ambao wanakuwa katika ndoa, tatizo hili lina uwezekano mkubwa wa kutibika sababu tiba zipo, na Tanzania kwa kushirikiana na Merck Foundation tumeungana kusaidia wanawake hawa wapate tiba," anasema Waziri Dorothy.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Merck Foundation Senator, Dk. Rasha Kelej, anasema taasisi hiyo imekuwa ikiendesha kampeni ya kupinga unyanyapaa kwa wanawake wenye matatizo ya ugumba na hata kufikia hatua ya kusomesha madaktari ili kupata ujuzi zaidi wa kuwatibu na kupata watoto. Anawahakikisha wanawake kuwa taasisi hiyo pia inafanya kazi na wake wa marais wa nchi 22 za Afrika ambao ni mabalozi wa kampeni ya 'more than a mother' ili kuzuia unyanyapaa kwa wanawake wagumba.

Aidha, wamekuwa wakitoa msaada wa vifaa tiba katika huduma za kiafya, pamoja na elimu kwa kinamama wagumba kuhudhuria kliniki ili wapimwe na kujua tatizo na kuanza tiba.

# Hata leo wanaume huwakataa, kuwakimbia pacha, eti mkosi

INATOKA UK.11

Pamoja na hayo anasema si vibaya watoto hao mapacha wakapewa bima za afya, wakapata nafasi ya kusoma bila kusumbuliwa kutokana na kwamba wanatoka katika familia zisizo na uwezo wa kuwahudumia.

### MSAADA HOSPITALI

Katika maadhimisho ya Siku ya Pacha mwaka huu, Diana anatembelea hospitali za Temeke, Ilala, Muhimbili na Mwananyamala za Dar es Salaam kusaidia.

Anatoa nguo za watoto, sabuni za kuogea na kufulia, mafuta ya kupaka, maziwa na pampasi vikiwa na thamani ya Shilingi 2,000,000, ukiwaendea waliojifungua mapacha Novemba 11, anasema Diana.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Hospitali ya Rufani ya Mwananyamala, Asia Mkini, anapongeza hatua hiyo na kusema ipo haja ya kufuatilia maisha ya kinamama na watoto wenye mapacha kuwasaidia.

Anarejea taarifa ya baadhi ya watu kumuomba mama wa watato watatu kutaka kuwachukua, akionya: "Mmesema wapo baadhi ya wamiliki wa vituo vya kuleta watoto yatima au walio katika mazingira magumu wakiwamo mapacha ambao baba zao wamewakimbia na wanarubuni mama zao ili kuchukua watoto, kama ni kweli wapo watu wanaofanya hivyo, wajue kwamba si sahihi," anasema Asia.

Aidha, anasema kama wamiliki wa vituo wana nia ya kweli, wafuate utaratibu ambao ni kupeleka maombi ustawi wa jamii na vilelezo vya shughuli zao na kusubiri ofisi ya ustawi ichunguze na kujiridhisha ili waruhusiwe kuchukua watoto.





## Wajasiriamali 1,500 wanolewa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAJASIRIAMALI zaidi ya 1,500 kutoka wilaya zote za Mkoa wa Singida, wamenufaika na mafunzo ya namna ya kuendesha biashara zao kwa ufanisi na weledi ili kujikwamua kiuchumi.

Mafunzo hayo yametolewa na shirika lisilo la kiserikali la Star Entrepreneur General kwa ufadhili wa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Singida, Aysharose Mattembe.

Katika hafla ya kuhitimisha mafunzo hayo mwishoni mwa wiki, Meneja wa shirika hilo, Yoel Mwenda, alisema wajasiriamali walifundishwa ufugaji kuku, kilimo biashara, usimamizi wa biashara, usindikaji wa mazao ya nafaka, mboga na matunda na utengenezaji wa sabuni za miche, batiki na kujitangaza ili kupata masoko.

Mbunge Mattembe aliziomba halmashauri zote mkoani Singida kutoa kipaumbele cha kuwapatia mikopo ya kuendeshea biashara zao wajasiriamali waliopata mafunzo ya ujasiriamali.

Alisema atazungumza na taasisi za fedha zinazotoa mikopo ili kuangalia uwezekano wa kutoa mikopo kwa wajasiriamali wakuze biashara zao na kujikwamua na umaskini.

"Ninataka kuona mwanamke wa Singida anayepika maandazi na vitumbua anamiliki kiwanda cha kuoka mikate. Ninataka kuona wanawake wa Singida wakimiliki migahawa mikubwa na wakimiliki viwanda vikubwa vya kukamua mafuta ya alizeti, inawezekana kabisa," alisema.

Mbunge huyo aliongeza kuwa mafunzo hayo yatakuwa endelevu na kila mwaka yatakuwa yanafanyika katika wilaya zote kwa lengo la kuunga mkono jitihada za serikali katika kuona kila Mtanzania anakuwa na shughuli ya kujiongezea kipato.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Singida, Naima Chondo, alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa kuwa serikali sasa inawekeza kwenye viwanda na wajasiriamali.

Alisema serikali kwa kutambua umuhimu wa wanawake katika kukuza uchumi wa mtu mmoja, jamii na taifa, imeondoa riba katika mikopo wanayokopeshwa wanawake kwa ajili ya kuanzisha shughuli za ujasiriamali.

# Dereva bajaji auawa kwa kucharangwa mapanga madai wizi wa ng'ombe

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma, limethibitisha kutokea mauaji ya kikatili ya dereva wa bajaji ambaye jina lake halijafahamika katika eneo la Nala, Kata ya Nala jijini Dodoma, baada ya kukatwa kwa mapanga akidaiwa mwizi wa ng'ombe.

Inadaiwa waliofanya tukio hilo ni wakazi wa eneo la Nala kwa madai ya kuchoshwa na vitendo vya wizi wa mifugo, ambayo huchinjwa baada ya kuibiwa na kupakiwa katika bajaji na kwenda kuuza nyama.

Akithibitisha tukio hilo, Kamanda wa Polisi mkoani Dodoma, Martine Otieno, alisisitiza raia kuacha kujichukulia sheria mkononi dhidi ya wahalifu wanaowabaini. Wawafikishe katika vyombo vya sheria.

Kamanda Otieno alisema Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wa tukio hilo ili kuwakamata waliosababisha kifo hicho, pia kuwasaka wezi wengine wanaofanya matukio ya wizi wa mifugo katika eneo hilo na kutumia usafiri wa bajaji kusafirisha nyama ya ng'ombe aliyechinjwa baada ya kuibwa katika mazizi ya wafugaji.

"Tunakemea vikali wananchi kujichukulia sheria mkononi ya kupiga watu wanaosadikiwa ni wahalifu hadi kuuawa, wananchi mnatakiwa kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi ili hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi ya wahalifu hao," alisema Kamanda Otieno.

Alisema polisi inaendelea na doria katika eneo hilo ili kuwakamata wahalifu, wakiwamo wezi wa mifugo.

Jeshi hilo pia linaendelea kufuatilia Mamlaka ya Mapato (TRA) ili kujua mmiliki wa chombo hicho ambacho kinafanya safari zake kutoka eneo la Kituo cha Mabasi Nanenane.

Akielezea tukio hilo, Diwani wa Nala, Elman Masila, alisema wakazi wa eneo hilo walianza kufuatilia michirizi ya damu toka eneo la tukio mpaka walipoiona bajaji hiyo na kuanza kuifukuza.

Masila alisema bajaji ilifika mahali na kushindwa kupanda kwenye mabonde ndipo wananchi hao walipomkuta dereva bajaji huyo anayekadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 20 hadi 30 na kuanza kumkata mapanga.

Alilitaja ni tukio la kusikitisha kwa kuwa wananchi hawakupaswa kujichukulia sheria mkononi, wangemkamata na kumpeleka katika kituo cha polisi ili atoe ushahidi na wahalifu wengine wakamatwe.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, George Simbachawene, akihutubia kwenye ufunguzi wa mkutano mkuu wa mwaka wa viongozi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) jana, unaoendelea jijini Dodoma kwa siku tatu. **PICHA: PAUL MABEJA**

# CBE yaagizwa kuanzisha mafunzo ya gesi, mafuta

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imekiagiza Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kuanzisha programu mpya za masomo zikiwamo za masuala ya sheria za mafuta na gesi, uwekezaji na kilimo biashara ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira la sasa.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alitoa maagizo hayo mwishoni mwa wiki iliyopita jijini hapa alipohutubia wakati wa mahafali ya 58 ya chuo hicho.

Alisema ili kuleta ushindani na vyuo vingine, CBE inapaswa kubuni programu mpya za masomo ambazo zitaisaidia kujitofautisha na wengine.

Naibu Waziri alibainisha kuwa hivi sasa mambo mengi yamebadilika, hivyo ipo haja kwa chuo hicho kuanzisha programu mpya za masomo ambazo zitakwenda kukidhi mahitaji ya soko la ajira la sasa.

"Mnaweza kuanzisha programu za masomo kama vile sheria za masuala ya mafuta na gesi, uwekezaji, kilimo biashara... hivi sasa serikali yetu imewekeza kiasi kikubwa cha fedha katika maeneo hayo," alisema Kigahe.

Alikipongeza chuo hicho kwa ubunifu ambao kimekuwa kinaufanya ikiwamo kuanazisha programu atamizi za biashara kwa ajili ya kulea na kuendeleza ubunifu mbalimbali unaoandaliwa na wanachuo.

Alisema programu hiyo itasaidia kujibu changamoto ya ajira kwa vijana ambao wamekuwa wanahitimu masomo ya vyuo vikuu na vyuo vya kati.

"Niwapongeze kwa kuwa wabunifu kuanzisha programu hii ambayo itawezesha vijana kubuni mawazo ya biashara na ninyi kuyalea ili baadaye iwe biashara kubwa na kujibu changamoto za kiuchumi na kijamii nchini," alisema Kigahe.

Awali Mkuu wa chuo hicho, Prof. Edda Lwoga, alisema pamoja na mafanikio waliyopata, wanakabiliwa na vikwazo mbalimbali ikiwamo uhaba wa mabweni kwa wasichana.

Alisema kutokana na hali hiyo, chuo kimetafuta eneo Kata ya Nzuguni ambako kinatarajia kufanya uwekezaji wa majengo ya chuo.

"Pia tunalo eneo katika mitaa ya Medeli ambako tunataka kujenga jengo la uwekezaji ambalo tutaingia ubia na sekta nyingine ili kujiongezea vyanzo vya mapato kwa ajili ya kuendesha chuo chetu," alisema.

Kuhusu programu atamizi za biashara kwa ajili ya kulea na kuendeleza ubunifu mbalimbali unaondaliwa na wanachuo, kiongozi huyo wa chuo alisema t ayari wameshasajiliwa vijana 185 na biashara zao kusajiliwa BRELA.

"Programu hii atamizi ya biashara inalenga kukabiliana na tatizo la ajira nchini, tunashindanisha vijana wetu wenye mawazo ya biashara pamoja na ubunifu mbalimbali ambao unaweza kujibu changamoto za kiuchumi na kijamii," alisema.

Alibainisha kuwa jumla ya wanachuo 792 wamehitimu katika fani mbalimbali za masomo katika mahafali ya 58 ya chuo hicho mwaka huu.





# Wasomi wahimizwa kutumia taaluma zao kuleta mabadiliko chanya

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

WASOMI nchini wametakiwa kuwa nyenzo ya mabadiliko chanya katika jamii kwa kutumia taaluma zao na maarifa waliyonayo kuwaelimisha wengine pamoja na kutatua changamoto zilizopo ndani ya jamii ili kuleta mabadiliko kwa jamii na Taifa kwa ujumla.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na washiriki kwenye kongamano la 20 la kumbukizi ya Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere lililoandaliwa na Chuo Kikuu cha Mzumbe Ndaki ya Mbeya na kufanyika jijini hapa. Mwenyekiti wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Joseph Butiku, alisema dhamira ya Mwalimu Nyerere kuweka misingi mizuri ya elimu ilikuwa ni kuwapika vijana kupitia fani mbalimbali, wajitegemee na kuendeleza wengine ili tuwe na Taifa la watu waliokomaa kiuchumi.

Mzee Butiku aliwasihi vijana walioko vyuoni na wanaohitimu kuenzi misingi ya Mwalimu Nyerere likiwamo suala la maadili, uzalendo, utu, kujali maslahi ya wengine, kulinda rasilimali za nchi pamoja na kuishi kwa kuzingatia misingi ya katiba ya nchi.

"Mwalimu Nyerere alitaka Taifa lenye watu wenye utu, alitaka maendeleo ya watu sio vitu, tena tunapozungumzia utawala bora ni maendeleo, niwatake wote tusimzungumze Mwalimu Nyerere kwa mazoea bali tumuenzi kwa vitendo," alisema Mzee Butiku.

Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Prof. Willium Mwegoha alisema vijana wanaohitimu vyuo wanapaswa kuwa wabunifu kwa kutumia ujuzi walioupata wakiwa shuleni kutengeneza fursa za ajira kwao na jamii inayowazunguka.

Alisema chuo hicho kinapika wataalamu wa masuala ya utawala hivyo katika kuendeleza misingi ya utawala bora aliyoanzisha Mwalimu Nyerere kinasisitiza somo la maadili kwa wanafunzi wake ili wawe wazalendo katika kulinda rasilimali za nchi.

Akifungua kongamano hilo Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Kanali Denis Mwila, alisema Baba wa Taifa aliacha alama kubwa katika utunzaji wa rasilimali za nchi hivyo ni muhimu taasisi za elimu kuwajengea uwezo vijana wa kutatua changamoto zao na za wengine kwa kutumia rasiliamali zilizopo.

Alisema idadi ya watu waliosikia hotuba za Mwalimu Nyerere inazidi kupungua na kubaki machapisho yake ambayo pia hayasomwi na vijana wengi na kushauri chuo hicho kuendelea kufanya kongamano hilo ili kuendelea kupandikiza mafunzo ya Mwalimu Nyerere kwa vijana hao.

Kongamano hilo lenye mada kuu isemayo, "Mtazamo wa Mwalimu Nyerere Juu ya Utawala Bora na Ulinzi wa Rasilimali za Taifa kwa Maendeleo Endelevu,"linalenga kuwahimiza vijana walioko shuleni na vyuoni kulinda na kuenzi mafunzo ya mwalimu nyerere kwa vitendo ili kuimarisha utawala bora na ulinzi wa rasilimali za Taifa.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Nangano iliopo Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, wakikinga maji kwenye bomba la shule hiyo mwishoni mwa wiki, ambalo limewekwa hivi karibuni ili kuwapunguzia adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RUWASA yawaokoa wakazi Masasi kuliwa na mamba

**Na Elizabeth John,**
LUDEWA

WAKAZI wa vijiji vinne vya Tarafa ya Masasi, wilayani Ludewa, mkoani Njombe wanatarajia kuondoka na changamoto ya kuliwa na mamba wanapokwenda kuchota maji katika Mto Ruhuhu baada ya serikali kupeleka mitambo ya kuwachimbia visima.

Akizungumza katika mkutano wa wananchi hao, Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Jeremiah Maduhu, alisema visima hivyo vitachimbwa katika kijiji cha Kiyogo Kata ya Masasi, Kata ya Manda vitachimbwa Kijiji cha Nsungu, Igalu na Mbongo kwa urefu wa mita 150 kwenda chini.

"Mh. Mbunge siku chache zilizopita uliahirisha mkutano wako hapa, ukasema unaenda kutafuta maji, naomba nikupongeze wewe na Rais wetu kwa kuhakikisha mitambo hii inaletwa katika kijiji hiki cha Kiyogo na kutatua changamoto hii kwa kuwa mradi huu ilitakiwa ukamilike muda mrefu," alisema Maduhu.

Alisema awali wananchi walitakiwa kupata maji kupitia mradi wa Lifua lakini kwa bahati mbaya mradi huo haufanikiwa kutoka maji ya kutosha kusambaza na maeneo mengine.

Maduhu alisema mitambo hiyo haitatoka katika kijiji hicho mpaka wahakikishe maji yamepatikana na wameshaandaa tangi la maji la lita 25,000 na vituo vya kuchotea maji sita.

Mmoja wa wananchi hao, Ester Makunguru alisema iliwalazimu kuweka uzio katika mto huo huku wakisindikizana na watu zaidi ya watano lakini pamoja na kufanya hivyo bado imekuwa changamoto kwa sababu mamba bado wanawavizia na kuwakamata.

"Ujio wa hii mitambo ni matumaini tosha kwamba tayari tumeshapata maji, tunamshukuru sana Rais wetu pamoja na mbunge kwani wameleta furaha katika kijiji chetu na kutuondosha katika ile Jehanam ya kuliwa na mamba kila kukicha misiba," alisema Makunguru.

Mbunge wa Jimbo la Ludewa, Joseph Kamonga, alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ni mama mwenye huruma kwa sababu ni muda mfupi tangu wananchi hao wapaze sauti zao na ametatua changamoto hiyo.

Kamonga alisema katika mradi wa Lifua ambao umeonekana kuwa na changamoto katika kuwafikia wananchi wengi tayari Rais aliagiza kuandikwa andiko ili kuuboresha na yuko tayari kutoa fedha za uboreshaji huo litakapokamilika.

# Mahakama yatupilia mbali rufani ya Kanisa KKKT

**Na Elizabeth John,** IRINGA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Iringa imetupilia mbali rufani ya kupinga hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Njombe ambayo ililikuta na hatia Kanisa la Kiinjili la kilutheri Tanzania Dayosisi ya Kusini baada ya gari lake kusababisha ajali iliyosababisha kifo cha Kaselida Mlowe eneo la Ruhuji mjini Njombe.

Akisoma hukumu ya kesi no 12 ya mwaka 2023 Msajili wa Mahakama Kuu Kanda ya Iringa, Maximilian Maleo, alisema mahakama imepitia sababu zote 10 zilizotolewa na upande wa mdaiwa na kujiridhisha kwamba hazina mashiko na kisha kuagiza upande wa mdaiwa ambaye ni kanisa kulipa fidia na gharama za kesi hiyo.

Imeelezwa kwamba kesi hiyo ya rufani ilifunguliwa na kanisa baada ya kutoridhishwa na hukumu iliyotolewa na Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Njombe, Lihad Chamshama, ambapo kanisa lilihukumumiwa kulipa fidia ya Sh. milioni 70.

Inaelezwa ajali hiyo ilitokana na uzembe uliofanywa na mdaiwa namba moja Rajab Kitwana, aliyekuwa dereva wa gari la kanisa aina Mercedes Benz Track lenye namba za usajili T 210-AHU na kugongana na gari la abiria aina ya hiace lenye namba za usajili T298 DNE katika mlima Ichunilo mjini Njombe Septemba 25, 2020.

Msimamizi wa mirathi wa familia ya marehemu, Sigrada Mligo, alifungua kesi No 2 ya mwaka 2022 ya madai ya fidia ya Sh. milioni 100 kutoka kanisa hilo lakini Mahakama ya Hakimu Mkazi Njombe ikasikiliza ushahidi kutoka pande zote mbili na kisha kutoa hukumu ya fidia Sh. milioni 70.

Awali upande wa mdaiwa ambaye ni kanisa haukuridhia na hukumu kuamua kufungua kesi ya rufani katika mahakama kuu kanda ya Iringa ambako rufani hiyo ilitupiliwa mbali baada ya mahakama kudai sababu zilizotolewa hazina mashiko.

Katika kesi hiyo upande wa madai uliwakilishwa na mawakili watatu akiwamo Emmanuel Chengula, Frank Ngafumika na Gervas Semgabo huku upande wa utetezi ambao ni kanisa ukiwakilishwa na wakili Marco Kisakali.

**Inaelezwa ajali hiyo ilitokana na uzembe uliofanywa na mdaiwa namba moja Rajab Kitwana, aliyekuwa dereva wa gari la kanisa aina Mercedes Benz Track lenye namba za usajili T 210-AHU na kugongana na gari la abiria aina ya hiace lenye namba za usajili T298 DNE katika mlima Ichunilo mjini Njombe Septemba 25, 2020.**

# Viongozi UWT wakumbushwa kuyaenzi mazuri ya waasisi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Ofisi ya Zanzibar, Tunu Juma Kondo, amewataka viongozi na wanachama wa umoja huo kuendeleza mambo mazuri yalioanzishwa na waasisi wa umoja huo.

Alisema viongozi waliopo wanafanya mambo mengi mazuri lakini pia kuna baadhi ya mambo yanahitaji kuendelezwa kwa faida ya jumuiya na wananchi kwa ujumla.

Aliyasema hayo jana katika Tawi la CCM Matariubeta, Wilaya ya Mjini Unguja, kuwataka wanawake wa umoja huo kuelimisha jamii kuachana na utumiaji wa dawa za kulevya, udhalilishaji na mmong'onyoko wa maadili katika jamii.

Hata hivyo alisema hatua hiyo itapelekea kupatikana viongozi wazalendo wenye uchungu wa nchi yao na kuepukana na ubadhirifu wa mali za umma, rushwa na ufisadi.

Wanawake wa umoja huo, walisema kuwa watahakikisha wanahamasisha malezi bora kwa jamii ili kuondokana na mmong'onyoko wa maadili na kupambana na vitendo vya udhalilishaji.

Mjumbe wa kamati tekelezaji UWT wilaya ya mjini Taiba Hamid Ameir, aliwataka wazazi na walezi kurejesha malezi ya pamoja ili mtoto yoyote anapofanya kosa la utovu wa nidhamu mzazi yoyote kumuadhibu ili kuwa fundisho kwa watoto wengine.

# Rais Samia atoa magari matano kwa Jeshi la Polisi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMISHNA wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad, amekabidhi magari matano kwa makamanda wa Jeshi la Polisi wa Mikoa mitano ya Zanzibar ili kurahisisha utendaji wa kazi wa jeshi hilo.

Akizungumza jana makao makuu ya jeshi hilo Zanzibar, katika hafla ya makabidhiano ya magari hayo yaliotolewa na serikali, Kamishna Hamad alisema magari hayo yanafanya jeshi hilo kupokea jumla ya magari 37 tangu uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Alisema jeshi hilo limo katika maboresho ili kurahisisha utendaji wa shughuli zake na magari hayo yatasaidia kutatua kero za wananchi.

"Kama kuna maeneo ambayo matatizo yanashindwa au kuchelewa kutatua kwa changamoto za usafiri, Rais Samia anatusaidia kutatua changamoto hizo, tunataka jeshi letu liwe la kisasa tukio linapotokea kusiwe na ucheleweshaji," alisema.

Alisema magari hayo yatasaidia askari wa jeshi hilo kufika katika eneo la tukio kwa wakati na kufanya kinachostahiki kwa mujibu wa taratibu wa jeshi na sheria.

Kamishna huyo aliwataka makamanda hao kuhakikisha magari hayo yanatumika kwa kazi iliyokusudiwa na si kuhakikisha yanatunzwa ili kudumu kwa muda mrefu.

Aidha alisema bado jeshi hilo linahitaji magari na pikipiki ili kurahisisha utendaji kazi wao kwa kuwa mpaka sasa bado kuna maeneo ambayo hayana magari hali inayopunguza kasi ya kuhudumia jamii.

"Kwa kipekee nimshukuru kwa mara nyingine tena Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuliangalia kwa jicho la pakee Jeshi la Polisi na kwa kweli anatufanyia makubwa sana ambayo yanasababisha tusiwe na kisingizio kingine," alisema.

Alisema Jeshi la Polisi lina deni kubwa kwa Rais Samia kwa mambo anayolifanyia na malipo yake ni kuhakikisha linawahudumia na kuwajibika kwa wananchi kwa sababu ndio wanaolipa kodi ambazo zimepelekea upatikanaji wa magari hayo.

Aliwataka makamanda hao pamoja na askari wote wa jeshi hilo kufanyakazi kwa weledi kwa kuzingatia maadili ya kazi ili kuonesha fadhila kwa Rais huyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Unguja, Gaudianus Kamungisha, alisema magari hayo yatasaidia kuongeza nguvu za kiutendaji na kuyatumia ambapo makosa mbalimbali ambayo yalikuwa na changamoto ya kutoyafikia kwa wakati sasa kuyafikia kwa ufanisi.

Naye Kamanda wa Mkoa wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Daniel Shila, alisema gari hiyo itarahisisha kufanya kazi kwa wepesi na haraka na kumpongeza Rais Samia kwa kulipatia vitendea kazi jeshi hilo ili kuwahudumia wananchi katika kutatua changamoto za kiusalama.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, William Timoth, alisema magari hayo yatawapa uwezo wa kuyafikia maeneo mengi ikizingatiwa kuwa Mkoa wa Kaskazini Pemba una changamoto ya usafirishaji wa magendo wa zao la karafuu ambalo ni zao la taifa.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (kushoto), akimwapisha Sadifa Juma Khamis kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kati Unguja, hafla iliyofanyika Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Serikali Zanzibar mbioni kuiboresha SUZA

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, amesema mipango ya serikali ni kukiboresha Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ili kuendana na dira ya mipango ya Zanzibar ya mwaka 2050.

Aliyasema hayo jana wakati akizindua baraza la nane la chuo hicho ambapo uzinduzi huo umefanyika Chuo cha Utalii Maruhubi Zanzibar.

Alisema serikali inahitaji kufanya uamuzi mkubwa lakini kutokana na taratibu za kimuundo na kisheria zilizopo lazima kupitia katika taasisi husika na kufuata mifumo inayotakiwa.

Alisema nia ya serikali kwa sasa ni kutoa vipaumbele kwa kada za ufundi na ujuzi kwa wanafunzi visiwani Zanzibar ili kuwa na wataalamu wengi katika kada ya kati.

Alisema SUZA imekuwa na mafanikio makubwa ya kuazisha programu mbalimbali na kiwango cha ufaulu wa wanafunzi kwa ngazi ya sekondari ni mkubwa lakini changamoto iliyopo wanashindwa kupata nafasi ya kuendelea na elimu ya juu katika chuo hicho.

"Serikali imekuwa ikichukua jitihada za kuboresha miundombinu na kuweka mazingira rafiki katika ngazi ya maandalizi, msingi na sekondari na ndio maana ufaulu umeongezeka hivyo SUZA lazima kuwa na mipango ya hawa ambao wanaofaulu watakapokuja katika safari yao ya elimu ya ngazi ya juu kuwa na nafasi ya kutosha," alisema.

Aidha alilitaka baraza hilo kukisaidia chuo hicho katika kutanua miundombinu ya chuo na kupokea wanafunzi wengi wa kada mbalimbali katika ngazi ya elimu ya juu.

Waziri huyo alisema SUZA ni chuo pekee cha serikali na kinachotoa huduma kwa wanafunzi wa ndani na nje hivyo lazima kutanua miundombinu na kuwa na kozi mpya.

"Waswahili wanasema fagio jipya huwa linafagia vizuri lakini fagio kongwe huwa linajua kona zote zenye taka, wajumbe mliomaliza muda wenu nyinyi ni fagio kongwe mnaijua vizuri SUZA na mipango ya serikali hivyo mlisaidie baraza hili jipya katika kusafisha na kulifanya jengo letu kuwa nadhifu, " alisema.

Naye Mkuu wa Chuo cha SUZA, Profesa Muhammed Makame Haji, alisema uzinduzi huo umewapa faraja ya kutimiza mipango waliojiwekea kwa kuwa baraza hilo ni chombo cha juu cha uongozi na muhimili wa chuo ambacho kinasimamia masuala yote ya chuo ikiwamo uongozi, matumizi ya fedha na kuleta maendeleo ya chuo na nchi.

Wakizungumza na waandishi wa habari baada ya hafla hiyo, wajumbe hao wapya wa baraza hilo, walisema, kuwa lazima Tanzania irejeshe hadhi na ubora wa kiwango cha elimu ili kupunguza msusuru wa vyuo vingi vya elimu ya juu hali ambayo imepelekea wanafunzi wengi baada ya kumalia elimu yao hawana ajira.

Dk. Ahmed Ramadhan Abeid ni miongoni mwa wajumbe hao, alisema kuwa hivi sasa kuna wahitimu wengi wa kiwango cha udaktari ambao ni wa 'mchongo' na uwezo wa kiutendaji ni mbovu ilikinganishwa na taaluma walionayo.

Naye Mjumbe anayewakilisha kundi la watu wenye ulemavu, Salma Haji Saadat, alisema jitihada kubwa zinafanyika kwa wanafunzi wenye ulemavu kufaulu masomo yao na wanafunzi 21 wenye ulemavu wamejiunga na elimu ya juu katika chuo hicho katika fani tofauti yakiwamo ya sayansi.

Aidha, alisema uwepo wao katika baraza hilo utasaidia ujumuishi kwa watu wenye ulemavu na kunasaidia katika kufanya mageuzi ya chuo kuajiri watu wenye ulemavu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**ABETH ALISTIDES CLEMENSI** amepotelewa na cheti cha kidato cha nne cheye namba S0637-0002 kilichotolewa Nyabiyonza shule ya Sekondari Wilaya ya Karagwe Mkoa wa Kagera.Taarifa za kupotea zilitolewa kituo cha Polisi Kahama,Mkoa wa Shinyanga na kupewa namba **PHQ/SH/KAH/630/2023.** Yeyote atakayekiona anaombwa kutoa taarifa kituo chochote cha Polisi.

## KUPOTEA KWA CHETI



**WILLINGTON-BIYA DEOGRATIAS MUKASA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0800/0185 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia LOYOLA HIGH SCHOOL mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi**:** **PHQ/DAR/TEM/42027/2023.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**Ndugu VICTOR E. KAGISA** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya pikipiki yenye namba za usajili MC 336 CEB ambayo ina majina ya JOHANES MWEMA DAUSON. Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **PHQ/KAG/BUK/3673/2023.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye.

**KUITWA SHAURINI**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Bukoba, Mjini Mkoa wa Kagera.**
**Shauri la madai namba 368/2023**
**Jina la Mdai Mathayo Blasio Budigama**
**Jina la Mdaiwa Egidius Tibesigwa Elizeus**

**Kwa Egidius Tibesigwa Elizeus.Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba madai ya Tsh 24,569,000**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 4,Mwezi 12 2023 saa 3;00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo.Na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa kwa shauri ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO.** Kama hautohudhuria siku hiyo na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini.Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw we kuwepo.
Hati imetolewa kwa Amri na Mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 01/11/mwaka 2023

01/11/2023
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA BUKOBA BUKOBA MJINI 38

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA KINONDONI MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI.....414......LA.....2010**

**MIDLASTER DANIEL NSWANZUGWAKO......MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**WILLY MUZE...............................................MDAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**
**WILLY MUZE**
**POPOTE ULIPO/MLIPO:**

MIDLASTER DANIEL NSWANZUGWAKO Amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 21/11/2023 saa 3:00 Asubuhi/Mchana mbele ya Mh SILLAS Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa

Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 17 Mwezi 11 , 2023

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

## KUPOTEA KWA TRANSCRIPT



**Ndugu IRENE B.MOSES** anatangaza kupotelewa na transcript ya chuo cha **TANZANIA PUBLIC SERVICE COLLEGE (TPSC)** kozi ya **ORDINARY DIPLOMA IN RECORDS MANAGEMENT** chenye namba ya usajili **DRM.07/11/T.382** kilichotolewa mwaka 2013,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa: PHQ/DAR/KIN/42327/2023**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**GIDO RAPHAEL KAYANI** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba **TAE 366905** iliyotolewa makao makuu mwaka 2020. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/UBU/4126/2023**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**TAJI JOSEPH GODSON** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya MITSUBISHI FUSO yenye usajili namba: T 796 AAL ,CHASSIS NAMBA: FK417K544199 na ENGINE NAMBA: 6D16663693. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA:**
**PHQ/ARU/ARU/6758/2023**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA SONGEA LILILOKO SONGEA**

**MAOMBI NAMBA 113/2023**

**NIKODEM VITALIS MWENDA...................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**LUKAS LUKAS NDOMBA**
**MARIA SIKUMOJA NGINDO**
**NICODEM NICODEM MWENDA............WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

Mjibu maombi wa pili na watatu, mnaarifiwa kuwa muombaji amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yenu. Hivyo basi mnatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wako, au wote kwa pamoja siku ya tarehe 30.11.2023 saa 5:00 asubuhi. Kumbuka pia nyaraka zote kuhusu mgogoro huu zipo hapa barazani kwa ajili ya kuleta hati yako ya utetezi.
Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusikiliza shauri hili bila kujali uwepo wako.

Imetolewa leo name na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 08/11/2023.

.................................
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**RUVUMA**

**FOMU MIRATHI - 2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 1747/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SAIDI SEIF JONGO wa Suna Kinondoni**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SHABANI JUMA JONGO**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 06 mwezi 12 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetokewa leo tarehe 17 mwezi 11 mwaka 2023.

HAKIMU

## KUPOTEA KWA VYETI



**TABIZUNA JUMA MPUNGA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1468/0024** kilichotolewa na CHAUME DAY SEKONDARI mwaka 2020. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S5896/0541** kilichotolewa na LUKAS MALIA HIGH SCHOOL mwaka 2023. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/TRT/TRT/2940/2023.**

## NAFASI ZA KAZI

Ualimu Masomo ya **Hesabu, Science, Kiswahili na Kiingereza.** Pia wanatakiwa walimu Wastaafu isizidi miaka mitatu (3) iliyopita kwa ajili ya ukaguzi.

**SIMU: 0783 298 900**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......123/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: HAMISI KIBWANA SAIDI wa MADIZINI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA MKEGANI HAMISI KIBWANA**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 4 Mwezi 12 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**

- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 16 mwezi 11 mwaka 2023

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MOROGORO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TANGA**
**Kituo cha MJINI TANGA**
**Mkoa TANGA**

**Usimamizi wa mirathi Na 184/ 2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU HAMADI HAMISI TWALIBU**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MARIAMU MUSSA MWILE**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/ maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 24 Mwezi 10 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**ZINGATIA;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 17 Mwezi 10 Mwaka 2023

HAKIMU
HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO TANGA MJINI

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA SONGEA LILILOKO SONGEA**

**MAOMBI NAMBA 17/2023**

**MALISELA DESDERIUS SANGA...................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**ZOOH MOHAMED KISALELE**
**COSMAS IVO KISALELE**
**OTHMAN MAJIMOTO............WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

Mjibu maombi wa pili na watatu, mnaarifiwa kuwa muombaji amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yenu. Hivyo basi mnatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wako, au wote kwa pamoja siku ya tarehe 30.11.2023 saa 2:30 asubuhi. Kumbuka pia nyaraka zote kuhusu mgogoro huu zipo hapa barazani kwa ajili ya kuleta hati yako ya utetezi.
Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusikiliza shauri hili bila kujali uwepo wako.

Imetolewa leo name na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 09/11/2023.

..........................................
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**RUVUMA**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SWALEHE RAMADHANI MATAULA** anatangaza kupotea kwa cheti cha form four chenye index No. **S2447-0056** kilichotolewa na baraza la Mitihani la Taifa kupitia **SEGALA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/DOD/9256/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOVIN DANIEL MASEKESA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 826 ABK** CHASSIS NO. **L J780026679,** ENGINE **NO. 2L2973963** AINA YA TOYOTA LANDCRUSEISER. KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFIA KITUO CHA KARIBU CHA POLISI **ARU/ARU/RB/268406/2023.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No.149 of 2023**
**In the matter of the estate of the late MWISUNGI CORNEL KIGOSI of Nyerere-Kilimani within Dodoma City.**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by PETROLINA EMANUEL MBASHA**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be on or before the 20 day of 12, 2023.
Dated at Dodoma this 20 day of 11, 2023.

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DICKSON AROBOGASTY TARIMO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA DBA QNC10** yenye usajili namba **T 334 DAJ** na CHASSIS NAMBA: **QNC100035091.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**SOG/RB/4357/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GUSTAV STEPHEN NGONYANI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **MITSUBISH CANTER** yenye usajili namba **T 721 DCY** na CHASSIS NAMBA: **FE517BD4011262.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**SOG/RB/4356/2023**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Iran yashauri mataifa kuitenga Israel

• Houthi nayo yatangaza uadui na Israel • Handaki laonekana chini ya hospitali



Miongoni mwa watoto njiti ambao wanahamishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kutoka Gaza kwenda Misri. **PICHA: AFP**

**Na Maulid Mmbaga**

KIONGOZI Mkuu wa Kidini wa Iran, Ayatollah Ali Khamenei, ametoa wito kwa mataifa ya Kiislamu yenye uhusiano wa kisiasa na Israel kukata mahusiano kwa kipindi fulani, akisisitiza kuwa jukumu kuu la serikali hizo ni kusitisha nishati na bidhaa nyingine kwenda Israel.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya nchini humo, Khamenei anaeleza kuwa kinachofanywa na Israel huko Gaza hakikubaliki, huku akieleza kwamba serikali za Kiislamu zinapaswa angalau kusitisha uhusiano wa kisiasa na Israel kwa muda, ikiwa ni wiki kadhaa baada ya kutoa wito wa vikwazo vya mafuta na chakula dhidi ya taifa hilo.

Aidha, wakati wa mkutano wa pamoja kati ya wanachama wa Umoja wa Nchi za Kiislamu na Umoja wa Nchi za Kiarabu uliofanyika katika mji mkuu wa Saudi Arabia, Novemba 11, mwaka huu mataifa ya Kiislamu hayakukubali kuiwekea Israel vikwazo vingi, kama ilivyoombwa na Rais wa Iran, Ebrahim Raisi.

**WATEKA MELI**

Wakati wito huo ukitolewa waasi wa Houthi wanaoungwa mkono na Iran nchini Yemen, wameteka meli inayomilikiwa na mfanyabiashara raia wa Israel katika bahari Nyekundu na kuipeleka pwani ya Yemen.

Hayo yanajiri siku chache baada ya wapiganaji hao kutishia kulenga mali zinazomilikiwa na Israel katika bahari hiyo kutokana na vita vinavyoendelea na wapiganaji wa Hamas katika Ukanda wa Gaza.

Msemaji wa Houthi, Yahya Saree, kupitia ukurasa wake wa X, (zamani Twitter) anathibitisha kutokea kwa tukio hilo la utekaji wa meli, huku mataifa ya Israel, Marekani na Japan yakilaani hatua ya wapiganaji hao kuteka chombo hicho.

> **Takriban watu 10 wameuawa katika shambulio la anga la Israel yanayoendelea, huku Wizara ya Afya inayoongozwa na Hamas ikisema kuwa ni watu 12 waliouawa.**

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, meli hiyo ilikuwa ikimilikiwa na kampuni ya Uingereza na shughuli zake zilikuwa zinaendelezwa na kampuni ya nchini Japan.

Hata hivyo msemaji wa Houthi anaeleza kuwa kundi hilo litaendelea kutekeleza operesheni za kijeshi dhidi ya kile anasema ni adui wa Israel hadi uchokozi dhidi ya Gaza na uhalifu mbaya dhidi ya ndugu zao wa Kipalestina utakapokoma.

**JAPAN**

Vile vile serikali ya Japan inalaani vikali kutekwa kwa meli hiyo ya mizigo ambayo imezua mvutano juu ya umiliki wake baada ya madai kuwa iko chini ya Japan huku wanamgambo wa Yemen wakidai kuwa inamilikiwa na Israel, lakini taarifa za Israel zinaeleza kuwa ni ya Uingereza.

Katibu mkuu wa baraza la mawaziri la Japan, anasema anashughulika ili meli hiyo iachiliwe. Huku Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu akiilaumu Iran, ambayo inaunga mkono wanamgambo wa Houthi, kwa utekaji nyara huo. Iran imekanusha madai hayo ya Israel kwamba wanashirikiana na wanamgambo wa Houthi.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje wa Iran Nasser Kanani, anasema waasi hao wanawakilisha mataifa yao na wanachukua hatua kwa ajili ya manufaa ya mataifa yao. Netanyahu anasema sio meli hiyo wala wafanyakazi 22 wa chombo hicho sio Waisraeli, akitaja kuwa kitendo hicho cha utekaji ni shambulio la Iran kwenye meli ya kimataifa.

Katibu Mkuu wa Baraza la Mawaziri la Japan, anasema "Kwa sasa mashirika, Wizara ya Uchukuzi na Mambo ya Nje wanakusanya taarifa na kushirikiana na nchi husika ili kuachiliwa mapema kwa meli hiyo na wafanyakazi wake".

Licha ya hayo, Israel inaahidi kumaliza kundi la Hamas ambalo linaoongoza Ukanda wa Gaza, hatua inayojiri baada ya wapiganaji hao wa Palestina kuwaua karibia raia 1,200 na kuwateka wengine karibia 240 Oktoba, mwaka huu kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa mamlaka ya Israel.

Mkurugenzi wa hospitali ya Indonesia kaskazini mwa Gaza, anasema kuwa takriban watu 10 wameuawa katika shambulio la anga la Israel yanayoendelea, huku Wizara ya Afya inayoongozwa na Hamas ikisema kuwa ni watu 12 waliouawa.

Msemaji wa wizara hiyo, Ashraf Al-Qudra ameliambia shirika la habari la AFP kwamba mbali na vifo hivyo, makumi ya watu walijeruhiwa.

**HANDAKI HOSPITALINI**

Katika hatua nyingine Jeshi la Israel limesambaza picha za awali zinazoonyesha shimo refu chini ya jengo la Hospitali ya Al-Shifa huko Gaza ambayo ilizingirwa na jeshi hilo siku za karibuni kutokana na madai ya kuwa na handaki chini yake linalokaliwa na Hamas.

Jeshi linasema video hiyo ilithibitisha madai kuwa Hamas ilikuwa na kituo cha amri chini ya hospitali hiyo, licha ya Hamas kukanusha madai hayo.

Kutokana na hali hiyo Shirika la Afya Duniani (WHO) limetoa wito wa watu kuhamishwa kutoka katika hospitali hiyo wakiita kama ni eneo la kifo. Wito huo wa WHO unatolewa huku kukiwa na ripoti inayosema kuwa, Israel na kundi la Hamas wamefikia makubaliano ya muda ya kusitisha mapigano na kuwaachilia huru mamia ya mateka.

Kupitia mtandao wa kijamii wa X, jeshi hilo linaeleza kuwa walifichua handaki lenye urefu wa mita 55 na kina cha mita 10 chini ya jengo la Hospitali ya Al Shifa.

Taarifa ya Jeshi la Israel inaeleza kuwa, vikosi vyake vilipata pia silaha na kugundua mlango mwingine ndani ya handaki hilo, japo hawakutoa taarifa juu ya kilichokuwapo ndani.

Kwa upande wa Hamas inasisitiza kuendesha mahandaki kadhaa katika ukanda wa Gaza japo inakanusha kumiliki mahandaki chini ya hospitali au sehemu nyingine za raia.

**MAAFA KWA WATOTO**

Inaelezwa kuwa siku ya watoto duniani inayoadhimishwa kila mwaka ifikapo Novemba 20, inayolenga kukuza haki za watoto, usalama, elimu, afya na furaha, imekuwa na mtazamo tofauti wakati huu huko Gaza baada ya zaidi ya watoto 5,500 kupoteza maisha kutokana na mashambulizi ya Israel katika ukanda huo.

Inaelezwa kuwa tangu Oktoba 7, mwaka huu mtoto mmoja wa Kipalestina anauawa kila baada ya dakika 10, au takribani mtoto mmoja kati ya 200 katika ukanda huo. Pia inabainishwa kuwa watoto wengine 1,800 hawajulikani waliko chini ya vifusi wengi wao wakidhaniwa kuwa wamekufa na kwamba wengine 9,000 wamejeruhiwa, wengi wao wakiwa na matokeo ya kubadilisha maisha, pamoja na kupitia kiwewe cha vita vingi.

WHO, inasema imefanikiwa kuwahamisha zaidi ya watoto njiti 30 kutoka katika hospitali kubwa huko Gaza, na kwamba linapanga kuwaondoa wafanyakazi wa hospitali hiyo katika kile inasema ni eneo la ukanda wa vifo.

***Chanzo mashirika ya kimataifa***

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### GRIEZMAN AWANIWA UNITED

KLABU ya Manchester United iko tayari kuongeza mara tatu mshahara wa Antoine Griezmann, 32, katika jitihada za kumsajili fowadi huyo wa Ufaransa kutoka Atletico Madrid katika dirisha la Januari. ***(El Nacional, via Mundo Deportivo)***

### SAMUEL ALENGWA JUVE

KLABU ya Juventus inaweza kuwa tayari kumuuza winga wa England, Samuel Iling-Junior, 20, ambaye amekuwa akilengwa na Tottenham Hotspur, katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Football Insider)***

### WILLIAMS KUTUA VILLA

KLABU ya Aston Villa inatafuta uwezekano wa kumnunua mshambuliaji wa Athletic Bilbao na Ghana, Inaki Williams, 29, Januari. ***(Football Insider)***

### FERNANDEZ KUZEEKEA UNITED

MSHAMBULIAJI wa Ureno, Bruno Fernandes, 29, amethibitisha kujitolea kwake kuendelea kuichezea Manchester United licha ya uvumi unaomhusisha na kuhamia Saudi Arabia. ***(90min)***

### NUSA ANUKIA CHELSEA

KLABU za Tottenham Hotspur na Chelsea zina nia ya kumnunua Antonio Nusa, 18, anayelengwa na Fulham ambaye ni mshambuliaji wa Norway anayewika katika Klabu ya Club Brugge. ***(Football Insider)***

### SANE KWA BARCA, MADRID

BARCELONA na Real Madrid zinafikiria kumnunua winga wa Bayern Munich na Ujerumani, Leroy Sane, 27. ***(Sport)***

### VINICIUS ATAFUTIWA MBADALA

KLABU ya Real Madrid inafikiria kumsajili mshambuliaji mwengine kwa mkopo au wa kudumu Januari baada ya Vinicius Jr, 23, kuumia akiwa na Timu ya Taifa ya Brazil, huku mshambuliaji wa RB Leipzig na Ujerumani Timo Werner, 27, akilengwa. ***(Sport - in Spanish)***

### EKITIKE ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inaweza kurejea tena kumnunua mshambuliaji wa Paris St-Germain, Mfaransa Hugo Ekitike, 21, katika dirisha la Januari. ***(Football Insider)***

### ZUBIMENDI ATAJWA BARCA

BARCELONA itafanya uhamisho wa kumsajili kiungo wa kati wa Hispania, Martin Zubimendi, 24, ambaye anahusishwa na Arsenal kutoka Real Sociedad msimu ujao. ***(Sport)***

### SMALLING OFA MPYA ROMA

AS Roma iko tayari kufikiria ofa kwa beki wa kati wa zamani wa England, Chris Smalling, 33, kwenye dirisha la Januari. ***(Gazzetta dello Sport)***

### DAVID ATAKIWA MILAN

KLABU ya AC Milan itajaribu kuimarisha safu yao ya ushambuliaji Januari na wanaweza kumnunua fowadi wa Lille na Canada, Jonathan David , 23. ***(Gazzetta dello Sport)***

## DONDOO ZA MAGAZETI YA ULAYA



# GAVI MAJANGA KWA HISPANIA, BARCELONA

**BARCELONA,** Hispania

KIUNGO wa kati wa Barcelona, Gavi, anakabiliwa na uwezekano wa kukaa nje ya uwanja kwa muda mrefu baada ya kupata jeraha la goti katika ushindi wa 3-1 wa Hispania wa kufuzu Euro 2024 dhidi ya Georgia Jumapili, kwa mujibu wa ESPN.

**Msemaji wa Shirikisho la Soka la Hispania (RFEF), alithibitisha kuwa tayari wameshatoa taarifa kwa Barca, ambao jana Jumatatu walimfanyia vipimo vyao wenyewe kwenye goti la kulia la Gavi.**

Kocha wa Hispania, Luis de la Fuente alifanya mabadiliko tisa kwenye kikosi cha 'La Roja' hao kilichoishinda Cyprus Ijumaa iliyopita, huku Gavi akiwa ni mmoja wa wachezaji wawili tu, pamoja na Robin Le Normand wa Real Sociedad, kushika nafasi zao.

Hata hivyo, alilazimika kutoka katikati ya kipindi cha kwanza baada ya kutua vibaya wakati akidhibiti mpira dakika chache baada ya kugongana na Luka Lochoshvili wa Georgia.

Gavi menye umri wa miaka 19, alikuwa akichechemea nje ya uwanja akiwa na madaktari wa timu ya Hispania, lakini sura ya uso wake ilionesha kuwa ana maumivu makubwa.

**Inaonekana ni jeraha baya, ana wasiwasi sana, tunasubiri vipimo vya uhakika...**

"Inaonekana ni jeraha baya," alisema De la Fuente akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo.

"Ana wasiwasi sana. Ni ushindi mchungu zaidi ambao nimewahi kuupata katika maisha yangu.

"Tunasubiri vipimo vya uhakika. Ataenda Barcelona na Mkurugenzi wa Michezo wa Hispania, Albert Luque kwa vipimo zaidi. Tumeharibiwa. Ni kana kwamba tumepoteza mchezo."

Aliongeza: "Gavi amevunjika, ameharibiwa ... hakufikiria kwamba mambo haya yanaweza kumtokea. Wakati hayajakutokea hapo awali, unaweza kufikiria kuwa hauko hatarini, lakini sisi ni dhaifu sana, anasikitika, sote tumevunjika. Hakuna maelezo zaidi ya haya yanayotokea maishani.

"Ndio, siku ngumu zaidi katika mchezo huu kwangu, yenye uchungu zaidi."

Wachezaji wa Hispania pia walionekana kufahamu ukubwa wa jeraha hilo, huku mwenzake wa Barca, Ferran Torres akishangilia bao lake ambalo lilifanya matokeo kuwa 2-1, kwa kushikilia jezi nambari 9 ya Gavi.

"Ulikuwa ushindi muhimu kumaliza awamu ya kufuzu vizuri, lakini ni hisia chungu kutokana na jeraha la Gavi," alisema Torres.

"Natumaini anaweza kupona haraka iwezekanavyo. Hatujui ukubwa wa jeraha hilo, tutalazimika kuona katika siku zijazo, lakini tukimjua Gavi, ni shujaa gani, tunafikiri inaweza kuwa mbaya."

Gavi amekuwa mchezaji muhimu kwa Barca na Hispania msimu huu, akikosa mechi mbili pekee - zote kwa klabu yake kwa kusimamishwa.

Lakini De la Fuente alikanusha mapendekezo kwamba jeraha hilo lilitokana na Gavi kucheza michezo mingi.

"Ni ajali, ni bahati mbaya. Haina uhusiano wowote na mkusanyiko wa michezo," alisema.

# JESUS KUICHEZEA BRAZIL DHIDI YA ARGENTINA



**SAO PAULO,** Brazil

GABRIEL Jesus anatarajiwa kuanza kuichezea Brazil dhidi ya Argentina Jumatano licha ya kuwa nje ya uwanja kwa takriban mwezi mmoja kutokana na jeraha la misuli ya paja.

Jesus aliitwa katika kikosi cha kocha, Fernando Diniz kwa mechi za kimataifa za Novemba licha ya kutoichezea Arsenal tangu Oktoba 24, mwaka huu alipopata jeraha la misuli ya paja dhidi ya Sevilla ambalo limemfanya kuwa nje ya uwanja tangu wakati huo.

Taarifa kutoka nchini Brazil zinaeleza kuwa viongozi wa Arsenal akiwamo Mkurugenzi wa Michezo, Edu wamekuwa wakiwasiliana na wenzao wa Brazil ili kuwasihi wamwache Jesus apumzike, lakini kilio hicho kinaonekana kutosikilizwa.

Jesus aliachwa nje ya kikosi kilichofungwa mabao 2-1 na Colombia mapema Ijumaa asubuhi, lakini jeraha la Vinicius Junior limeacha pengo kwenye safu ya ushambuliaji ya timu hiyo ambayo Diniz anatarajia kuijaza na Jesus.

Mshambulizi huyo wa Arsenal alihusika katika mazoezi ya timu Jumamosi, akipangwa pamoja na washambuliaji wengine na sasa wanatarajiwa kuanza pambano Jumatano dhidi ya wapinzani wa jadi, Argentina.

Diniz hivi majuzi alisisitiza kuwa alichukua "hatari" iliyokadiriwa katika kumwita Jesus, ambaye utimamu wake umekuwa ukifuatiliwa kwa karibu.

"Ninamwamini mchezaji na yeye kuwa hapa," alisema bosi huyo wa Brazil. "Nilizungumza na Gabriel hakuja hapa bila kupanga, alisema anajisikia vizuri na tayari alikuwa akifanya mambo siku kumi kabla ya mchezo wa kwanza na siku 15 kabla ya mchezo wa pili.

"Tuliona ni hatari ya kuvutia kumleta hapa, yuko katika hali nzuri, tunafanya mambo kwa umakini mkubwa, alipofika tu tulimfanyia kipimo kipya cha MRI, tunamshughulikia kwa umakini mkubwa.

"Ikiwa yuko katika hali nzuri, atapatikana dhidi ya Argentina. Kama sivyo, nina uhakika ilikuwa muhimu sana kwa Gabriel kuja hapa."

# Fernandes amtaka Neves United

**MANCHESTER,** England

BRUNO Fernandes amewahimiza Manchester United kufanyia kazi nia yao ya kumnunua kiungo wa Benfica, Joao Neves.

United wamekuwa wakimchunguza mara kwa mara kinda huyo mwenye umri wa miaka 19 na walihudhuria huku aking'ara katika ushindi wa hivi majuzi wa Benfica wa mabao 2-1 dhidi ya Sporting CP, wakimtazama kijana huyo pamoja na maskauti kutoka Arsenal na Liverpool.

Kiwango bora cha Neves msimu huu kimemfanya aitwe mara mbili katika Timu ya Taifa ya Ureno.

Kinda huyo aliingia akitokea benchi kwa dakika tano za mwisho za ushindi wa mabao 5-0 Oktoba dhidi ya Bosnia & Herzegovina na kuona dakika nyingine tatu dhidi ya Liechtenstein Alhamisi.

Alipoulizwa kuhusu nia ya United kumnunua Neves, Fernandes alikiri kuwa angependa kuona kijana huyo akijiunga naye Old Trafford, lakini tu ikiwa kocha Erik ten Hag ataona mustakabali wake.

"Lazima awe kocha wa Manchester United ambaye anasema kama ana nafasi katika timu au la," alisema Fernandes akiwaambia waandishi wa habari.



"Ni mchezaji mzuri, sijui kama angekuwa na nafasi au la, inategemea na kocha na mawazo yake. Lakini ni mchezaji bora na mtoto bora, mtaalamu sana. Atakuwa na mustakabali mzuri popote atakapokuwa.

"Ningependa kuwa naye kando yangu, kwa sababu ana ubora na atakuwa na mustakabali mzuri. Inategemea yeye. Ninachotaka zaidi ni bora kwake."

Neves si mchezaji pekee wa Kimataifa wa Ureno kwenye rada za United, kwani beki wa kati wa Benfica, Antonio Silva, ambaye alicheza dakika zote 90 dhidi ya Liechtenstein, pia anafuatiliwa, pamoja na mlinzi wa Sporting CP, Goncalo Inacio.

Baada ya kuanza vibaya msimu huu, ambao umekuwa ukiandamwa na majeraha, United wanataka kuimarisha kikosi chao Januari na wameandaa orodha ndefu ya walengwa.

# Onana ajiondoa Cameroon

**DOUALA,** Cameroon

SHIRIKISHO la Soka la Cameroon, limethibitisha kuwa mlinda mlango wa Manchester United, Andre Onana, amejiondoa kwenye kikosi hicho baada ya kupata jeraha kwenye mchezo dhidi ya Mauritius.

Onana alichechemea mwishoni mwa ushindi wa mabao 2-0 wa timu yake huku ripoti zikieleza kuwa ni tatizo la misuli, lakini Cameroon sasa imethibitisha kuwa amepata jeraha kwenye sehemu zake za siri, moja ya mifupa mitatu kwenye nyonga.

"Shirikisho la Soka la Cameroon linafahamisha umma kwamba mchezaji Andre Onana alijeruhiwa wakati wa mechi dhidi ya Mauritius mnamo Novemba 17, 2023 huko Douala na hayumo katika kikosi cha 'Simba Wasiofugika' huko Benghazi," ilisema taarifa.



Onana sasa atarejea Manchester kwa ajili ya kuangaliwa zaidi na klabu yake ya Man United ambayo itarejea uwanjani baada ya mapumziko ya kimataifa wakiwa na safari ya kwenda Everton Jumapili ijayo.

Iwapo Onana atashindwa kupona kwa wakati, Kocha wa United, Erik ten Hag, anaweza kulazimika kumchezesha Altay Bayindir katika mechi yake ya kwanza kwa klabu hiyo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uturuki anasubiri mechi yake ya kwanza baada ya kujiunga kutoka kwa United Fenerbahce kwa ada ya pauni milioni sita.

Bayindir alikuwa kwenye mechi ya kimataifa Jumamosi wakati timu yake ikipata ushindi mkubwa wa 3-2 dhidi ya Ujerumani, na jana Jumanne ilikuwa ikicheza na Wales.

Ten Hag tayari ana uwezekano wa kumkosa Marcus Rashford, ambaye alichechemea wakati England ikishinda 2-0 dhidi ya Malta.

Lisandro Martinez, Luke Shaw, Tyrell Malacia, Jonny Evans, Casemiro, Christian Eriksen, Amad Diallo na Rasmus Hojlund wote ni majeruhi.

# GBT YAITUNUKU BETWAY KINARA WA KUTII KANUNI MICHEZO KUBAHATISHA

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), ambayo ndiyo yenye mamlaka ya kuratibu na kusimamia shughuli za michezo ya kubahatisha na ubashiri, imeitunuku Kampuni ya Betway Tanzania cheti kwa kuibuka kinara wa kuzingatia kanuni zinazosimamia michezo hiyo nchini.

Tukio hilo lilifanyika hivi karibuni wakati GBT ikiadhimisha miaka 20 tangu kuanzishwa kwake kwa sherehe kubwa iliyohudhuriwa na wadau wa sekta hiyo.

Wakati wa tukio hilo moja ya mambo makubwa ilikuwa ni bodi hiyo kutambua mchango wa makampuni yanayoendesha shughuli za michezo ya kubashiri kwa kutoa vyeti vya ubora kwa makampuni hayo.

**Betway Tanzania iliibuka kama kampuni inayoongoza kwa kuzingatia kanuni zinazosimamia michezo ya kubahatisha na ubashiri Tanzania na kupewa cheti cha utambuzi na bodi hiyo.**

Licha ya kuwa na miaka miwili pekee nchini Tanzania, Betway imeendelea kuwa kampuni bora katika michezo ya kubahatisha na kubashiri na kuwa mfano bora kwa makampuni mengine yanayoendesha shughuli za ubashiri nchini.

Akitoa shukrani zake kwa kupata utambuzi huo, Jimmy Masaoe, Meneja Uendeshaji wa Betway Tanzania, ameliambia Nipashe jana kuwa, kutambuliwa kwao kunaendana sambamba kabisa na falsafa ya biashara ya kampuni hiyo ambayo inahimiza ubashiri wa kistaarabu katika nchi zote walizomo.

"Tunajivunia sana kwa kutambuliwa na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha nchini kama kampuni inayozingatia zaidi kanuni za michezo ya kubahatisha na ubashiri hasa tukizingatia uwapo wetu wa muda mfupi katika soko la Tanzania ikilinganishaa na makampuni mengine ambayo yamekuwapo kwa muda mrefu zaidi.

"Hii inathibitisha dhamira yetu isiyoyumba ya sisi kuwajibika na kuhimiza wateja wetu kuwajibika kwa kubashiri kistaarabu," alisema Masaoe.

Wakati Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania ikiadhimisha miongo miwili ya kusimamia sekta hiyo, imeendelea kuonesha mchango wake mkubwa katika uchumi wa nchi.

GBT imetoa mchango muhimu katika kuongeza mapato ya kikodi yanayotokana na michezo ya kubahatisha, ambayo yameongezeka kutoka Sh. bilioni 2.8 mwaka 2006/07 hadi Sh. bilioni 170.4 mwaka 2022/23. Zaidi ya hayo, bodi imechangia sana ongezeko la ajira kwa vijana kwa kuvutia wawekezaji 67 katika sekta hiyo.

Kupitia kutambua juhudi za makampuni yenye dhamira njema kama Betway Tanzania, GBT inachangia kikamilifu kuweka mazingira wezeshi na yatakayoleta matokeo chanya kwa taifa kupitia michezo ya kubahatisha na kubashiri.



Meneja Uendeshaji wa Betway Tanzania, Jimmy Masaoe, akipeana mkono na Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania, James Mbalwe hivi karibuni jijini Dar es Salaam, baada ya kupokea cheti cha pongezi kwa Betway kama kampuni inayozingatia zaidi kanuni za michezo ya kubahatisha na ubashiri nchini. **MPIGAPICHA WETU**

## Pamba yaing'oa KenGold kileleni

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Pamba FC imeing'oa kileleni KenGold kwa kuicharaza mabao 2-1 katika mechi ya raundi ya 11 ya Ligi ya Championship iliyochezwa Uwanja wa Nyamagana, jijini Mwanza juzi.

Mabao ya washindi yaliwekwa wavuni na Mudathir Said na Anicet Revocatus, huku la kufutia machozi la KenGold likifungwa na Edgar William.

Kipigo hicho cha KenGold kimeiondoa kileleni mwa msimamo ikishuka hadi nafasi ya pili ikibaki na ponti 23, Pamba ikipanda hadi nafasi ya tano ya msimamo na pointi zake 21.

TMA sasa imerejea tena kileleni baada ya kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya FGA Talents, mechi ikichezwa Uwanja wa Black Rhino uliopo Karatu, Arusha.

Yalikuwa ni mabao ya Abdulaziz Shahame na Seleman Bwenzi yaliyoipeleka TMA juu ya msimamo baada ya kudondoshwa wiki iliyopita, ikifikisha pointi 25.

Mbeya Kwanza nayo ilishindwa kukwea juu ya msimamo wa ligi hiyo wiki iliyopita baada ya kuchakazwa mabao 3-1 dhidi ya Biashara United, katika mchezo uliochezwa Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza.

Mabao ya washindi yalitumbukizwa nyavuni na Boban Zirintusa aliyefunga mawili na Malulu Masunga akifunga moja.

Kwa ushindi huo, Biashara United inapanda hadi nafasi ya sita ikiwa na pointi 18, huku Mbeya City ikibaki na pointi zake 23 sawa na KenGold, ikiwa kwenye nafasi ya tatu.

Kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, Pan African ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Green Warriors.

## Taifa Stars, Morocco ni ushindi tu leo

INATOKA UKURASA 24

zuri kupambana kusaka ushindi katika mchezo wetu huo, tunakutana na Morocco ambayo ipo kwenye ngazi ya juu," alisema Manula.

Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Morocco, Walid Regragui, alisema anafurahi kufika Tanzania salama na wako tayari kwa ajili ya kusaka ushindi katika mchezo huo dhidi ya Tanzania utakaochezwa leo.

Alisema wamefanya maandalizi ya mchezo huo kama ilivyo kwa mechi nyingine na wanahitaji kufuzu na kusonga mbele hali itakayowalazimu kushinda mechi ya leo.

"Ili mtu afuzu basi mechi ya kesho ni muhimu kuhakikisha anapata ushindi, tunaenda kucheza mechi kwa umakini mkubwa, hatuwezi kuangalia tunacheza na timu ya aina gani.

"Tanzania hatuwachukulii kama wako daraja la chini, tuna waheshimu na wanajituma sana na ukizingatia wanacheza mbele ya mashabiki wao watapambana kwa ajili ya kupata matokeo mazuri," alisema Walid.

## Simba yatoa sababu kuchelewa kupata kocha

INATOKA UKURASA 24

kwa sababu viongozi wanapambana kutafuta mtu sahihi wa kuja kuchukuwa nafasi ya Robertinho," alisema Ahmed.

Aliwatoa hofu mashabiki kuwa timu kwa sasa iko sehemu salama chini ya makocha wao Daniel Cadena na Selema Matola, ikiendelea na maandalizi ya mchezo wa kwanza wa hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumamosi ya wiki hii.

"Benchi la ufundi na wachezaji wanatambua umuhimu wa kupata ushindi katika mchezo wetu wa Novemba 25, mwaka huu, tutakaocheza nyumbani kusaka alama tatu ili kujiweka katika nafasi nzuri katika kundi letu.

"Lakini kwa upande wa Wanasimba tumeongea nao wamekubali kusahau yaliyopita hayana faida na zaidi kutengeneza yaliyopo mbele yetu ili kupata furaha katika mchezo huo," alisema Ahmed.

# Michezo

Jumanne Novemba 21, 2023

Nipashe




Gavi majanga Hispania, Barca UKURASA 21

LEO NI LEO!...



Baadhi ya wachezaji wa Taifa Stars, wakishangilia ushindi wa mechi iliyopita ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia 2026 dhidi ya Niger, iliyopigwa nchini Morocco Jumamosi iliyopita. Stars itaikaribisha Morocco katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam leo katika mchezo mwingine wa kuwania kufuzu fainali hizo. **MPIGAPICHA WETU**

# STARS, MOROCCO NI USHINDI TU LEO

**Na Saada Akida**

## Makocha wote watamba, wachezaji wasema ni raha kucheza na timu kubwa, lakini...

WAKATI Taifa ya Stars ikishuka Uwanja wa Benjamin Mkapa leo kuikaribisha Timu ya Taifa ya Morocco kwenye mechi ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia 2026, makocha wa timu hizo kila mmoja ametamba kukiandaa kikosi chake vizuri kwa ajili ya kupata matokeo bila kujali anakutana na timu ya aina gani.

**Stars inashuka dimbani leo saa 4:00 usiku kusaka ushindi wa pili ikiwa na morali ya hali ya juu baada ya kushinda mchezo wa awali Jumamosi iliyopita ikiwa ugenini kwa kuichapa Niger bao 1-0 kwenye mechi iliyopigwa nchini Morocco.**

Niger inacheza mechi zake za nyumbani nchini Morocco kutokana na viwanja vya kwao kushindwa kukidhi vigezo vya Fifa.

Kuelekea mechi hiyo ya leo, Wamorocco hao jicho lao wanalielekeza zaidi kwa Mbwana Samata, nahodha wa Taifa Stars na Simon Msuva ambaye amewahi kucheza ligi nchini Morocco katika Klabu ya Difaa El Jadida Wydad Casablanca.

Hata hivyo, Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Adel Amrouch, akizungumza na Nipashe jana alisema wanaenda kucheza na timu kubwa na anaimani ya kufanya vizuri leo katika uwanja wa nyumbani.

Alisema anaimani na kikosi alichonacho ingawa kuna baadhi ya wachezaji walikuwa majeruhi, lakini kikubwa kilichopo kwake ni kuangalia makosa yaliyopo kwa sababu maandalizi waliyofanya ya mechi iliyopita ni tofauti na mechi dhidi ya Morocco.

"Mechi ya Niger tulijitahidi kutumia wachezaji na vipaji tulivyokuwa navyo, tunatumia mfumo kulingana na aina ya wachezaji ambao tuko nao, hatuwezi kutoa mfumo ambao aina ya wachezaji tuliona utakuwa unawapa mzigo mkubwa.

"Hata ukiangalia katika viwango vya soka tunaona jinsi Tanzania ilipo, lakini pia timu ya taifa hatuna muda mwingi wa kukaa na wachezaji, hali ambayo tunalazimika kujiandaa kulingana na mechi iliyopo mbele yetu," alisema na kuongeza:

"Tunawaheshimu wapinzani wetu, ninaimani na vijana wangu wanauwezo wa kupambana na kupata matokeo mazuri katika mchezo wetu wa kesho (leo) dhidi ya Morocco," alisema Adel.

Alisema wana timu nzuri na wachezaji wenye uwezo wa kufunga bao na kutengeneza nafasi, hivyo wanaendelea kupambana kuwapa mbinu ili kuweza kutumia nafasi hizo kuzaa mabao.

Naye mwakilishi wa wachezaji wa Stars, Aishi Manula, alisema wanaenda kukutana na timu kubwa na wamejiandaa vizuri kwa ajili ya kupambani taifa kusaka ushindi.

Alisema ni mechi kubwa na ngumu ambayo itaonesha ushindani mkubwa kwa sababu ya ukubwa wa wapinzani ambao wanakutana nao leo.

"Wachezaji wakubwa wanapenda kucheza na timu kubwa, tumejiandaa vi-

INAENDELEA UKURASA 23

# Simba yatoa sababu kuchelewa kupata kocha

**Na Saada Akida**

LICHA ya awali kusema mrithi wa Robertinho Oliveira, atapatikana angalau siku 10 kabla ya kucheza mechi ya kwanza ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Asec Mimosas, uongozi wa Simba sasa umevunja ukimya kwa kueleza kilichokwamisha mchakato huo wa kumpata kocha mkuu mapema.

Makocha wengi wanahusishwa kuja kuchukua nafasi ya Robertinho akiwamo Sven Vandenbroeck, Abdelhak Benchikha, ambaye alikuwa chaguo la kwanza, lakini imeshindikana kutokana na dau kubwa analohitaji na mwingine Fernando Da Cruz pamoja na Radhi Jaidi.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema hawataki kufanya jambo hilo kwa haraka kwa sababu wanahitaji kufanya maboresho makubwa kwa kuleta mtu ambaye wataenda naye sawa kwenye mipango yao ya muda mrefu.

Alisema wanahitaji kuwa watulivu katika mchakato huo wa kupata mtu aliyekuwa sahihi ambaye atakuja kwa ajili ya kwenda nao katika njia moja, hivyo wanahakikisha wanapata kocha bora mwenye vigezo walivyoweka.

"Tumeona kuna makocha wengi wakitajwa akiwamo Benchikha ni kocha mzuri, hakuna sehemu viongozi wa Simba wamemtaja, mchakato umechelewa kwa sababu ya kutohitaji kupata kocha baada ya mechi mbili tunamwondoa.

Kuepukana na hilo tumelazimika kuwa makini katika mchakato huu, mashabiki wanatakiwa kuwa wavumilivu



INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >